# PAZIA LIMEONDOLEWA

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Pazia Limeondolewa

**Tafsiri ya Kiswahili ya:** Kashful-Ghitaa (Kiurdu)
Kashful-Ghitaa (Swahili Translation)

**Mwandishi**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri**

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1898
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-784-6
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

(Jalada la chapa ya mara ya kwanza)

اے قادر خُدا

اس گورنمنٹ عالیہ انگلشیہ کو ہماری طرف سے نیک جزا دے

اور اُس سے نیکی کر جیسا کہ اُس نے ہم سے نیکی کی۔ آمین

# کَشفُ الغِطَاء

یعنے

ایک اسلامی فرقہ کے پیشوا مرزا غلام احمد قادیانی کی طرف سے بحضور گورنمنٹ عالیہ اُس فرقہ کے حالات اور خیالات کے بارہ میں اطّلاع اور نیز اپنے خاندان کا کچھ ذکر اور اپنے مشن کے اصولوں اور ہدایتوں اور تعلیموں کا بیان اور نیز اُن لوگوں کی خلاف واقعہ باتوں کا ردّ جو اس فرقہ کی نسبت غلط خیالات پھیلانا چاہتے ہیں۔

اور یہ مؤلف

تاج عزّت جناب ملکہ معظمہ قیصرۂ ہند دام اقبالہا کا واسطہ ڈالکر بخدمت گورنمنٹ عالیہ انگلشیہ کے اعلیٰ افسروں اور معزز حکّام کے باادب گذارش کرتا ہے کہ براہ غریب پروری و کرم گستری اس رسالہ کو اوّل سے آخر تک پڑھا جائے یا سُن لیا جائے

یہ رسالہ تالیف ہو کر ۲۷ دسمبر ۱۸۹۸ء کو مطبع ضیاء الاسلام قادیان میں باہتمام حکیم فضل الدین صاحب مالک مطبع کے طبع ہوا

تعداد ۳۵۰

(Tafsiri ya jalada la chapa ya mara ya kwanza)

**Ee Mungu Mweza,**

**Uipatie serikali hii tukufu ya Kiingereza malipo bora kutoka kwetu na Uitendee wema kama ilivyotutendea wema. Amin**

# PAZIA LIMEONDOLEWA

Yaani

kutoka kwa Kiongozi wa dhehebu moja la Kiislamu, Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, kwa serikali tukufu kuhusiana na taarifa juu ya hali na fikira za dhehebu hilo, na vilevile kumbukumbu kiasi fulani ya ukoo wangu na maelezo ya kanuni, maagizo na mafundisho ya misheni yake; na mkanusho wa maneno, yaliyo kinyume cha ukweli, ya watu wanaotaka kueneza dhana mbaya dhidi ya dhehebu hilo.

Na Mwandishi huyu

**akipitia Mheshimiwa Malkia Muadhama, Kaisari wa India, idumu heshima yake, anawaomba kwa adabu maafisa wakubwa na watawala waheshimiwa wa serikali tukufu ya Kiingereza kwamba kwa heshima na hisani kijitabu hiki kisomwe au kisikilizwe tangu mwanzo mpaka mwisho.**

Kijitabu hiki kikiandikwa tarehe 27 Desemba 1898 kilichapwa katika matbaa ya Dhiaul Islam, Qadian, chini ya usimamizi wa mwenye matbaa Bw. Hakiim Fadhlud Din.

Idadi: 350

# MAELEZO YA MWENEZI

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian, alipodai kuwa ametumwa na Mwenyezi Mungu akiwa Imam Mahdi na Masihi Mau'udi, wakati huo Waingereza walikuwa wanatawala nchini India. Ilivyo desturi ya viongozi wapotovu wa dini kumpinga aliyetumwa na Mwenyezi Mungu, masheikh wengi walifutuka na kuukilia, bali wakajibidiisha, kumtweza Seyidna Ahmad[as] na kumwaziri.

Sheikh mmojawapo, jina lake Muhammad Husain Batalawii, aliyekuwa anamsifu sana zamani Seyidna Ahmad[as] kwa sababu ya kuitetea Islam na kuhakikisha ukweli wa dini hii tukufu kwa hoja imara na ishara za kimbingu, ghafula akageuka kuwa adui wake mkali, baada ya yeye kudai kutumwa na Mwenyezi Mungu, na akamtolea fatuwa ya kumkufurisha.

Isitoshe, akabutadi kuipelekea serikali ya Kiingereza habari za kuongopea dhidi ya Seyidna Ahmad[as] kwamba yu mwasi wa serikali, kwani anaamini kwamba Mahdi atapigana vita na Wakristo na kueneza Islam kwa ncha ya upanga na atamwaga sana damu nchini.

Sheikh huyo pia akachapisha kijarida kimoja kwa Kiingereza na kuipelekea serikali, ambamo akakana itikadi ya ujaji wa Mahdi atakayemwaga damu. Akaandika sina itikadi kama hii.

Katika kitabu hiki kilicho mkononi mwenu, Seyidna Ahmad[as] amethibitisha kwa hoja madhubuti kwamba

sheikh huyo ni ngole mkubwa, kwani yeye ndiye anayeitakadi yale aliyonasibisha kwangu, bali mimi ndimi niipingaye itikadi hiyo. Seyidna Ahmad[as] akaishauri serikali kuwakusanya sheikh huyo pamoja na masheikh wenzake na kumwambia kueleza mbele ya masheikh wenzake itikadi yake, kuhusiana na Mahdi, aliyoandika ndani ya kijarida chake. Bila shaka hataweza kueleza itikadi hiyo aliyoandika katika kijarida, kwani yeye pamoja na masheikh wenzake wote wanaamini ujaji wa Mahdi atakayemwaga damu na kupigana na Wakristo ili kuwasilimisha kwa upanga.

Seyidna Ahmad[as] alitangaza madhumuni ya kijarida kwa Kiurdu ndipo masheikh wenzake wakatambua ujanja wa kiongozi wao, Sheikh Muhammad Husain, na hapo Sheikh huyo akapata fedheha kubwa baina ya wenzake. Na ndipo bishara ya Seyidna Ahmad[as] ikatimia barabara iliyotabiri kwamba Sheikh atapatwa na fedheha ya aina ile ile jinsi alivyonifedhehesha.

Kitabu hiki kimefasiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, nami nimeidurusu kwa uangalifu kwa kulinganisha na matini ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain alipanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fomati yake. Mwenyezi Mungu Awabariki wote waliohusiana na kutoa tafsiri hii.

Jamil R. Rafiq

Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan. 28 Januari 2021

**Kwa heshima kubwa ya Mhashamu Muadhamu Malkia, Kaisari wa India – idumu heshima yake – nawaambia watawala wetu waheshimiwa wakisome kijitabu hiki kwa makini tangu mwanzo mpaka mwisho.**

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[1] نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ[2]

Kwa kuwa mimi, niitwaye Ghulam Ahmad, mwanaye Mirza Ghulam Murtadhaa, mkazi wa Qadian, wilaya ya Gurdaspur, ni Kiongozi wa dhehebu moja maarufu linalopatikana katika sehemu nyingi za Panjab, na vilevile wafuasi wa Jumuiya yangu wapo ndani ya wilaya nyingi za India, Haidarabad, Bombay, Madras na katika nchi za Uarabuni, Shamu na Bukhara pia, kwa hiyo nimeonelea itafaa niandike kijitabu hiki kwa lengo hili kwamba maafisa wakubwa wa serikali hii yenye hisani wapate kujua habari zangu na fikara za Jumuiya yangu. Kwani, naona kwamba dhehebu hili jipya linaendelea kupanuka siku hadi siku katika nchi hizi kiasi hiki kwamba maafisa wengi wenyeji, machifu wenye heshima, wenye ardhi na majengo na wafanyabiashara maarufu wameshajiunga katika dhehebu hili na wanaendelea kujiunga. Kwa hiyo,

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Waislamu wa fikara ya kawaida na masheikh wao wanayo inadi na husuda dhidi ya dhehebu hili. Na yumkini kwa husuda hii, mambo kinyume cha ukweli yafikishwe serikalini. Kwa sababu hiyo nimenuia kwamba kupitia kijitabu hiki niiarifu serikali hii yenye hisani habari zangu za kweli na mafundisho ya misheni yangu.

Sasa, kwa kutoa maelezo bayana nagawa mambo haya katika matawi matano. La kwanza, mimi ni nani na natokana na ukoo gani? Kuhusu hii, naona kudhihirisha kiasi hiki kwamba ukoo wangu ni ukoo wa watawala na wazee wangu walikuwa watawala wa nchi na viongozi shupavu walioangamia mara moja katika zama za utawala wa Masingasinga. Ingawa hisani ya Serikali ya Kiingereza ni juu ya wote, lakini wazee wangu walifanyiwa hisani zaidi, kwani walisalimika na mateso makali kwa kuingia katika amani wakiondoka maisha yenye hatari. Baba yangu, Mirza Ghulam Murtadhaa, alikuwa chifu na mwenye sifa nzuri katika maeneo haya; na maafisa wakubwa waliandika kwa kusisitiza kwamba yeye alikuwa mwenye ikhlasi ya kweli kwa serikali hii. Na baba yangu alikuwa akipewa kiti cha heshima katika baraza la Gavana, na daima maafisa wakubwa walimheshimu. Na kwa hulka zake za ukarimu, wakati mwingine viongozi wa wilaya na

divisheni walikuwa wakimtembelea nyumbani mwake, kwani machoni mwa viongozi wa Kiingereza alikuwa chifu mwaminifu. Na nina yakini kwamba serikali haitasahau kamwe huduma yake hii kwamba katika hali ngumu ya mwaka 57 [1857] alisaidia serikali zaidi ya uwezo wake kwa kuinunulia farasi hamsini, na maaskari wapanda farasi hamsini toka miongoni mwa jamaa na marafiki zake; kati yao baadhi ya jamaa zake wakipigana na wafisadi kwa ushujaa katika India wakatoa maisha yao. Na ndugu yangu, marehemu Mirza Ghulam Qadir alishiriki katika vita ya Timmu na akasaidia kwa bidii sana. Ilmuradi, hivyo ndivyo wazee wangu hao walivyothibitisha uaminifu wao mbele ya serikali kwa damu yao, kwa mali zao, kwa uhai wao na kwa huduma zao za kufululiza. Basi, kwa huduma hizo nina yakini kwamba serikali tukufu haitauchukulia ukoo wetu kama raia wa kawaida na haitapoteza haki yake hii iliyoishathibitika wakati wa fitina kubwa. Sir Lepel Griffin pia amewataja baba yangu na ndugu yangu, Mirza Ghulam Qadir, katika kitabu chake, *Taariikh Raisane Panjab* – Historia ya Machifu wa Panjab. Na hapa chini naandika baadhi ya barua za viongozi wakubwa ambamo huduma za baba yangu na za kaka yangu zimetajwa kiasi fulani.

**نقل مراسلہ (ولسن صاحب) نمبر ۳۵۳**

تہور پناہ شجاعت دستگاہ مرزا غلام مرتضیٰ رئیس قادیان حفظہٗ

عرائضہ شما مشعر بریاد دہانی خدمات و حقوق خود و خاندانِ خود بملاحظہ حضور ایں جانب در آمد۔ ماخوب میدانیم کہ بلاشک شما و خاندان شما از ابتدائے دخل و حکومت سرکار انگریزی جان نثار و فاکیش ثابت قدم ماندہ اید و حقوق شما دراصل قابلِ قدر اند۔ بہر نہج تسلی و تشفی دارید۔ سرکار انگریزی حقوق و خدمات خاندان شما ہرگز فراموش نہ خواہد کرد۔ بموقعہ مناسب بر حقوق و خدمات شما غور و توجہ کردہ خواہد شد۔ باید کہ ہمیشہ ہوا خواہ و جان نثار سرکار انگریزی بمانند کہ دریں امر خوشنودی سرکار و بہبودی شما متصور است۔

فقط

المرقوم ۱۱؍ جون ۱۸۴۹ء

مقام لاہور انارکلی

## Tafsiri ya barua ya J. M. Wilson, Na. 353

Kwa Mheshimiwa Mirza Ghulam Murtadhaa, Chifu wa Qadian.

Nimesoma kwa makini barua yako ambamo umenikumbusha huduma za siku zilizopita na haki zako na za ukoo wako. Natambua vizuri kwamba tangu mwanzo wa serikali ya Kiingereza, bila shaka wewe na ukoo wako m raia wenye ikhlasi, waaminifu na imara, na kwamba haki zenu kwa kweli zinapaswa kuthaminiwa. Kwa vyovyote utumaini na kutulia kwamba serikali ya Kiingereza haitasahau kamwe haki za ukoo wako na

huduma zao zitakazofikiriwa wakati mwafaka. Yawapasa kuendelea kuwa raia wenye kuitakia heri serikali ya Kiingereza na kujitolea kwake, kwani ndani yake kuna furaha ya serikali na ustawi wenu.

Imeandikwa 11 Juni 1849,
Anarkali, Lahore.

نقل مراسلہ

**(رابرٹ کسٹ صاحب بہادر کمشنر لاہور)**

تہور وشجاعت دستگاہ مرزا غلام مرتضیٰ رئیس قادیان بعافیت باشند

از آنجا کہ ہنگام مفسدہ ہندوستان موقوعہ ۱۸۵۷ء از جانب آپ کے رفاقت و خیر خواہی و مدددہی سرکار دولتمدار انگلشیہ در باب نگاہداشت سواران و بہمرسانی اسپان بخوبی بمنصہء ظہور پہنچی اور شروع مفسدہ سے آج تک آپ بدل ہواخواہ سرکار رہے اور باعث خوشنودی سرکار ہوا۔ لہٰذا بجلدوے اس خیر خواہی اور خیر سگالی کے خلعت مبلغ دو صد روپیہ کا سرکار سے آپ کو عطا ہوتا ہے اور حسب منشاء چٹھی صاحب چیف کمشنر بہادر نمبری ۵۷۶ مورخہ ۱۰ اگست ۱۸۵۸ء پروانہ ھٰذا باظہار خوشنودی سرکار و نیک نامی و وفاداری بنام آپ کے لکھا جاتا ہے۔

مرقومہ

تاریخ ۲۰ ستمبر ۱۸۵۸ء

**Tafsiri ya barua ya Mhe. Robert Cast, Kamishna wa Lahore**.

Kwa Mheshimiwa Mirza Ghulam Murtadhaa, Chifu wa Qadian.

Katika uasi wa mwaka 1857, tulipata habari za urafiki wako na kuitakia kwako heri serikali ya Kiingereza na msaada wa maaskari na farasi. Na tangu kuanzia mchafuko hadi sasa ukawa mwenye kuitakia heri serikali, jambo lililosababisha furaha ya serikali. Hivyo, ajilani unatuzwa na joho na Rupia mia mbili kwa sababu ya wewe kuitakia heri na wema serikali. Na sawa na utashi wa Kamishna Mkuu, barua hii Na. 576 ya 10 Agosti 1858 unaandikiwa kudhihirisha uradhi wa serikali na wema wako na uaminifu wako.

Imeandikwa:
20 Septemba 1858

نقل مراسلہ

**فنانشل کمشنر پنجاب**

مشفق مہربان دوستان مرزا غلام قادر رئیس قادیان حفظۂ آپ کا خط ۲ ماہ حال کا لکھا ہوا ملاحظہ حضور اینجانب میں گذرا۔

مرزا غلام مرتضی صاحب آپ کے والد کی وفات سے ہم کو بہت افسوس ہوا۔ مرزا غلام مرتضیٰ سرکار انگریزی کا اچھا خیر خواہ اور وفادار رئیس تھا۔

ہم آپ کی خاندانی لحاظ سے اسی طرح عزت کریں گے جس طرح تمہارے باپ وفادار کی کی جاتی تھی۔ ہم کو کسی اچھے موقعہ کے نکلنے پر تمہارے خاندان کی بہتری اور پابجائی کا خیال رہے گا۔

المرقوم ۲۹، جون ۱۸۷۶ء

الراقم سر رابرٹ ایجرٹن صاحب بہادر فنانشل کمشنر پنجاب

**Tafsiri ya barua ya Sir Robert Egerton, Kamishna wa Fedha, Panjab.**

Rafiki yangu mpendwa, Ghulam Qadir, Chifu wa Qadian, nimesoma kwa makini barua yako ya tarehe 2 ya mwezi huu.

Tumesikitika sana kwa kifo cha baba yako, Mirza Ghulam Murtadhaa aliyekuwa Chifu mwaminifu na mwenye kuitakia heri serikali ya Kiingereza.

Kwa sababu ya ukoo wako tutakuheshimu jinsi alivyoheshimiwa baba yako mwaminifu. Wakati mwafaka ukipatikana tutakumbuka kuhusu ustawi na ubora wa ukoo wako.

Iliandikwa 29 Juni 1876

Mwandishi, Sir Robert Egerton, Kamishna wa Fedha, Panjab

Hizo ndizo habari za baba na ndugu yangu. Na kwa kuwa maisha yangu ni kama ya mtu wa dini na wa kidarweshi, kwa hiyo mimi niliendelea kidarweshi kushughulikia kuitakia heri serikali ya Kiingereza. Tangu miaka 19 takriban nimetumia wakati wangu kuchapisha vitabu ambamo mmeelezwa kwamba Waislamu wanapaswa kuihudumia kwa ukweli wa moyo serikali hii na wanapaswa kuthibitisha utii na uaminifu wao zaidi kuliko kaumu zingine. Nami kwa lengo hili niliandika baadhi ya vitabu katika lugha ya

Kiarabu na vingine katika lugha ya Kiajemi na kuvisambaza mpaka nchi za mbali. Na ndani ya hivyo vyote nikawasisitizia Waislamu mara kwa mara na kuwalekeza kwa kutoa sababu za kiakili kwamba waitii serikali kwa moyo wote. Na vitabu hivyo vilipelekwa Uarabuni, Shamu, Kabul na Bukhara. Ingawa nasikia kwamba baadhi ya masheikh wasio na maarifa kwa kuvisoma hivyo wamenikufurisha na wameyachukulia maandishi yangu kwamba nina uhusiano wa ndani na wa siri na serikali ya Kiingereza, na kana kwamba napata zawadi fulani kutoka serikali kama malipo ya maandishi hayo. Lakini nimepata kujua kwa yakini kwamba mioyo ya baadhi ya wenye busara imeathirika vizuri sana na maandishi hayo na wameshatubia itikadi hizo za kihuni walizokuwa wameshikilia kinyume cha shabaha za serikali hii. Maandishi yangu ya kidini yaliyokuwa dhidi ya mapadri yameleta athari nzuri, waila jinsi nilivyowaita Waislamu kwa nguvu kuitii serikali hii na jinsi nilivyowakosoa mara kwa mara masheikh wa mpakani wasio na maarifa ambao kila siku wanasababisha fitina bila sababu na kuwahamasisha Waafughani kuleta upinzani, maandishi hayo yenye nguvu ya kuisaidia serikali ya Kiingereza hayakuwa yenye kuvumuliwa na Waislamu wenye chuki na wasio na maarifa. Na sasa upande mmoja wenye lubu wanapokuta madhumuni ya kuisaidia dini katika maandishi yangu na upande mwingine

wanaposikiliza nasaha zangu hizi kwamba serikali hii itiiwe na kuombewa heri, basi hawawezi kunidhania vibaya. Na kwa nini wanidhanie hivyo, kwani ni kweli kabisa kwamba Waislamu wameamuriwa na Mungu na Mtume[saw] kwamba waitii serikali yao kwa uaminifu. Nimeshaeleza kwa utondoti amri hizo za sheria katika vitabu vyangu. Sasa serikali inaweza kutafakari kwamba ikiwa baba yangu alikuwa kweli anaitakia heri serikali na ndugu yangu pia alifuata nyayo zake na mimi pia naendelea kutoa huduma hiyo kwa kalamu yangu tangu miaka kumi na tisa, basi mambo yangu yanawezaje kuwa yenye kuleta mashaka. Ujana wangu wote umepita kwa njia hiyo na sasa ni muwele na ukingoni mwa uzee na nimeshakaribia miaka sitini. Anadhulumu mtu yule anayenichukulia kuwa hatari kwa serikali. Siwezi kukanusha kwamba nimeishaandika vitabu kuhusu mambo ya dini pia, wala sikatai kwamba maandishi yangu yamesambazwa pia dhidi ya itikadi za mapadri, ambayo hawawezi kuyapenda sawa na fikira zao za kidini. Lakini kwangu mimi, nia yangu njema inanitosha Anayojua Mungu. Na hitilafu yangu ni tofauti na namna ya upinzani wa Waislamu wa kawaida. Sipendi kabisa chuki izidishwe katika mambo ya dini kiasi hiki kwamba shambulizi la wapinzani likichukuliwa kuwa hatia ya kisheria waadhibiwe na serikali au wabughudhiwe. Bali, msimamo wangu ni huu kwamba katika mijadala ya dini inapaswa

kushikamna na subira na hulka. Ndiyo sababu wakati Waislamu wa kawaida, kwa kumwadhibisha mwandishi wa Kitabu *'Ummahaatul Muminiin'*, walipozipeleka kumbukumbu serikalini kwa kupitia Anjuman Himayate Islam, sikuafikiana nao. Bali nilipeleka kumbukumbu kinyume chao, nami nikaandika wazi wazi kwamba katika mambo ya dini likitokea jambo la kuhuzunisha, hapo fundisho la Islam ni kusamehe na kutolititilia maanani. Kurani inatuongoza waziwazi kwamba mkiudhiwa na maneno makali katika maongezi ya kidini, msifike mahakamani kama wenye moyo finyu bali mshikamane na subra na hulka njema. Kurani imetusihi waziwazi kwamba muwatendee Wakristo kwa upendo na hulka njema na wafanyieni wema. Naam, kwa nia safi na kwa njia ya kuhurumia na kwa lengo la kusambaza ukweli na kwa nia ya kujenga suluhu, mijadala ya kidini haina ukinzani.

Tawi la pili lihusianalo na misheni yangu ni mafundisho yangu. Tangu miaka kumi na tisa ninasambaza mafundisho yangu. Kisha nikachapisha mafundisho hayo kwa muhtasari katika tangazo la 20 Mei 1898 na vilevile katika tangazo la 27 Februari 1895. Na vitabu hivyo na matangazo, vyote hivyo vikichapwa vimeshapata kujulikana sana katika Panjab na India. Muhtasari wa mafundisho hayo ni huu tu kwamba Mwaminini Mungu kuwa Mmoja, Asiye na mshirika na wahurumieni waja wa Mungu, na muwe

wanadamu wenye mienendo mizuri na fikira njema. Muwe hivi kwamba ufisadi wowote na shari zisiweze kuukaribia moyo wenu. Msiseme uongo, msizushe wala msimwudhi yeyote kwa ulimi wala kwa mkono, na mjiepushe na dhambi ya kila aina na mjizuie na tamaa za nafsi. Jaribuni kwamba muwe na moyo safi na kutokuwa na shari. Serikali ile, yaani serikali ya Kiingereza, ambayo chini ya utawala wake mali, heshima na uhai wenu upo salama, muwe waaminifu na watiifu wake kikweli. Na inapaswa kwamba kawaida yenu iwe kuwahurumia wanadamu wote. Na lindeni mikono yenu na ndimi zenu na mawazo yenu ya moyoni na kila njama mbaya, njia za kufitinisha na uhaini. Mcheni Mungu na Mwabuduni kwa moyo safi. Na jiepusheni na dhuluma, ujeuri, wizi wa mali ya Umma, rushwa, kuwanyima wengine haki zao na upendeleo usiofaa. Na mjiepushe na kukaa na waovu na yazuieni macho kutazama kwa tamaa ya mwili, na lindeni masikio kusikiliza misengenyo wala msinuie kumwudhi na kumhasiri mtu wa dini nyingine yoyote na taifa lolote na wa kundi lolote. Na muwe mwenye kumsihi kila mmoja kwa ukweli wa moyo. Na inapaswa kwamba wafitini, washari, majambazi na wenye miendendo mibaya wasikaribie vikao vyenu. Mjiepushe na kila uovu na jaribuni kutenda kila wema. Yapasa mioyo yenu isiwe na ulaghai, mikono yenu na dhuluma, macho yenu na uchafu, na isipate katu kufanyika baina yenu njama ya maovu na maasi, na

yapasa mjaribu sana kumtambua Mungu ambaye kumpata ni kuokoka hasa, na kukutana Naye ni kupata uhuru fika. Mungu Yule Anamdhihirikia yule mtu tu anayemtafuta kwa ukweli wa moyo na upendo. Yuajidhihirisha kwa yule anayekuwa Wake. Mioyo iliyotakata ndiyo makao makuu yake ya kifalme; na ndimi zilizosalimika na kuongopa, kutukana na kuropoka ni pahala pa wahyi wake. Na kila anayejipoteza katika ridhaa yake huwa dhihirisho la kudura yake ya kimuujiza. Huu ni mfano wa mafundisho yale inayofundishwa Jumuiya hii tangu miaka 19. Kwa hiyo, nina yakini kwamba wafuasi wa Jumuiya hii ni wamchao Mungu, watiifu na wenye shukurani kwa serikali ya Uingereza kwa moyo na wenye kuwahurumia wanadamu. Hawanayo jazba ya kihuni, hawana sifa za kinyama. Kama wakuu wa serikali wavumulie takilifu kidogo na wayasome kwa umakini maandishi yangu ya miaka 19, basi watakuta katika vitabu vyangu vingi mafundisho yale niliyoyaandika kwa mfano. Mfuasi yeyote hawezi kubaki mfuasi mpaka aone kauli na amali za kiongozi wake zaafikiana. Basi, kama kauli yangu ni ile niliyoandika mfano wake na vitendo vyangu viwe kinyume chake, hapo wenye busara wanawezaje kubaki kuniamini, ilihali sehemu kubwa ya Jumuiya yangu ni ya watu wenye akili na wasomi. Miongoni mwao baadhi yao wana vyeo vya heshima katika serikali, yaani wakuu wa kata, Makamishna wadogo

wa ziada, mawakili, madaktari, madaktari wadogo wapasuaji na waheshimiwa viongozi machifu na wafanyabiashara wa Panjab ambao majina yao nayachapisha mara kwa mara. Kila mwenye akili anaweza kufahamu kwamba hakuna uovu zaidi kuliko huu kwamba mafundisho ya mtu yawe tofauti na vitendo vyake vya kisiri. Basi, je watu wenye moyo mwema na wenye busara waweza kuungana na mshari kama huyo hata kwa kitambo kidogo? Kwa serikali jambo hili ni la kutuliza sana kwamba wanajumuiya wangu sio majahili, wahuni, waovu, mahabithi na wenye mienendo mibaya. Bali hao ni watu wema na wanajulikana kwa mienendo yao myema, ambao wengi wao hutambuliwa serikalini kuwa wenye mienendo mizuri, tabia yao nzuri, moyo safi na wenye kuitakia heri serikali, na wana vyeo vya heshima serikalini. Ushahidi aliochapisha Sir Seyid Ahmad Khan KCSI kunihusu mimi wakati wake wa mwisho, yaani siku chache kabla ya kifo, kutokana nao serikali tukufu inaweza kutambua kwamba mtu huyu mwenye busara na mtambuzi wa sifa za watu amependa njia yangu na mwenendo wangu. Hivyo, naandika maneno yake ndani ya maelezo ya pembeni.[3]

---

[3] **"Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian"**

Tangazo alilotoa Bwana Mirza tarehe 25 Juni 1897, ndani yake Bwana Mirza ameandika sentensi nzuri sana juu ya kuitakia heri

Sasa kimuhtasri, mafundisho yangu ni haya haya niliyoyaandika hapa kama mfano. Na Jumuiya yangu ni kundi la watu wa heshima, wapole na wenye mienendo

---

serikali ya Kiingereza na kuitii. Sawa na rai yetu kila Mwislamu aliye raia wa serikali ya Kiingereza anapaswa kuwa hivyo alivyoandika Bwana Mirza. Kwa hiyo twaichapisha sentensi hii katika gazeti letu. Bwana Mirza ameandika kwamba "Shambulio nililofanywa mimi kwa kuitakia heri serikali ya Kiingereza, shambulio hili pia ni kutia fitina tu. Sultani wa Rumi anazo haki zake, lakini haki za serikali hii pia zinahakikia juu yetu, na kutoshukuru ni aina ya ulaghai.

Enyi msiojua, sifa ya serikali ya Kiingereza haielezwi kwa kalamu yangu kiunafiki kama ninyi; bali najua kwa itikadi yangu na yakini kwamba kwa kweli ulinzi wa serikali hii kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu ni ulinzi wa Mwenyezi Mungu kupitia serikali hii. Ninaweza kuwa na uhakikisho gani zaidi wa serikali hii ya utawala wa amani, kuwa serikali ya amani kwamba Mwenyezi Mungu Ameanzisha Jumuiya hii tukufu katika utawala wa serikali hii. Kwangu mimi, watu hao ni wasaliti wa hali ya juu ambao wanawasifu sana bila kustahili watawala mbele yao, wanajinyenyekeza mbele yao, na wakifika nyumbani wanasema kwamba mtu anayeishukuru serikali hii ni kafiri. Kumbukeni, na kumbukeni sana, kwamba tunayotendea serikali hii sio kiunafiki, na laana ya Allah iwe juu ya wanafiki. Bali imani yetu ni hii hii iliyomo moyoni mwetu. Ali Garh Institute Gazette pamoja na Tahdhibul Akhlak, 24 Julai 1897.

mizuri. Siwezi kudhani kamwe kwamba kuhusiana nao serikali idhihirishe rai hii kwamba watu hao ni wa kuhatarisha au wa kushukiwa kulingana na vitendo na mwenendo wao. Hii ni bahati nzuri ya Jumuiya yangu kwamba wahuni, majahili na waovu hawakuelekea kwangu. Bali Jumuiya yangu imejaa watu waungwana, waheshimiwa, wasomi, maafisa wananchi na wafanyakazi wa serikali wenye madaraka ya juu. Na Waislamu wenye mawazo finyu ya chuki na ujahili ambao ni wahuni, waliotawaliwa na jazba zao za nafsi na wenye mawazo madogo hawahusikani na Jumuiya hii, bali wanaiona kwa uchoyo na inadi na wanashughulikia njama za kutuudhi na wanatuita makafiri.

Tawi la tatu la mambo yangu ambalo kuifikishia serikali ni muhimu sana, ni madai yangu ya kiufunuo niliyodai yaihusuyo dini, ambayo baadhi ya washari wanaotaka kujifaidisha wanayaandika katika majarida na magazeti yao kwa sura ya hatari na wanahadithia

---

Makala hiyo kuhusu kuitakia heri serikali ya Kiingereza nilichapisha wakati ambapo Sheikh Muhammad Husain wa Batala na watu wengine waliandika makala kumsifu Sultani wa Rumi, na kwa sababu ya mimi kuitakia heri serikali hii walinikufurisha. Bwana Sir Seyid Ahmad Khan alijua vizuri jinsi ninavyoitakia heri serikali ya Kiingereza na ni mtu mpenda amani. Ndiyo sababu katika kesi ya Daktari Clark nilimwandikisha Bwana Seyid kama shahidi mtetezi wangu. Mwandishi.

kinyume cha hakika ilivyo na kuzusha mambo. Nina yakini kwamba sina haja ya kuelezea kwa kuhakikisha kwa hoja mbele ya serikali yangu yenye busara kwamba Mungu Aliye Mwumba wa dunia hii na Mwenye kutoa matumaini na bishara za kudumu za maisha ya baadaye Anayo kanuni ya kudura yake tangu kale kwamba kwa kuwaongezea maarifa watu walioghafilika Anawafunulia baadhi ya waja wake; na Anaongea nao na kuwadhihirishia ishara zake za kimbingu. Na hivyo wakimwona Mungu kwa macho ya kiroho na wakijaa yakini na upendo wanapaswa wawavute wengine pia kwenye chemchemi hii ya uzima wanamokunywa, ili watu walioghafilika wakimpenda Mungu wapate wokovu wa kudumu. Na kila wakati inapopoa huba ya Mungu duniani na kwa kughafilika, utakaso wa kweli wa batini unapovurugika, hapo Mungu Akimfunulia mmojawapo miongoni mwa waja wake Anamwinua kwa kutakasa mioyo. Basi, katika zama hizi kwa kazi hii aliyemtuma baada ya kumtakasa kwa mkono wake ndiye mimi. Nami nimeinuliwa kwa kupanda mioyoni mbegu za utakaso wa kweli kama yule Mja Mtakatifu aliyesimama kabla ya miaka elfu moja mia tisa takriban tangu leo katika zama za utawala wa Kirumi katika vijiji vya Galilaya kwa kutoa wokovu wa kweli. Na kisha katika serikali ya Pilato, baada ya kusumbuliwa sana na Wayahudi akalazimika kuhama nchi zile sawa na suna ya kale ya Mungu. Akaja India ili awafikishie Wayahudi ujumbe wa Mwenyezi Mungu waliofika katika nchi hizo

wakati wa mtawanyiko wa Babeli. Na hatimaye katika umri wa miaka mia na ishirini akiondoka dunia hii isiyo ya kudumu na kumlaki Mpendwa wake, na akalipatia eneo la Kashmiri fahari ya kudumu kwa sababu ya kaburi lake tukufu. Bahati nzuri ilioje ya Srinagar, Anmuzah na mtaa wa Khanyar ambapo ndani ya udongo wake akauweka mwili wake mtukufu huyo mwanamfalme wa kudumu, nabii mtukufu wa Mungu. Akawapa wakazi wengi wa Kashmir hisa katika uzima wa milele na wokovu wa kweli. Daima jalali ya Mungu iwe pamoja naye. Amin. Basi, kama yule nabii mwanamfalme alivyokuja duniani kwa unyonge na umaskini, akaionyesha dunia mfano wa unyonge, umaskini na ustahimilivu, ndivyo ambavyo katika zama hizi Mungu Alitaka kwamba sawa na mfano wake Anitume niliye kutika ukoo wa kifalme na watawala na kidhahiri pia ninafanana na hali za yule mwanamfalme nabii wa Mungu, kwa watu hawa ambao wameshaenda mbali na hulka za kimalaika. Basi sawa na mfano huo, Mungu Alinitakia nikae duniani kwa unyonge na umaskini. Kulikuwa na ahadi tangu zamani katika Neno la Mungu kwamba mtu kama huyo azaliwe duniani. Kwa hiyo, Mungu Aliniita jina Masihi Mau'udi, yaani mtu anayefanana na Isa Masihi kihulka. Mungu Alimpa Masihi[as] makazi katika utawala wa Kirumu na utawala ule haukumdhulumu kwa kusudi, lakini Wayahudi waliokuwa kaumu yake, walimdhulumu sana, kumfedhehesha mno na kujaribu kuihakikishia serikali

kuwa yu mwasi. Lakini najua kwamba serikali yetu hii iliyo serikali ya Uingereza – Mungu Aiweke salama – ni safi kuhusiana na kanuni za uadilifu kuliko Warumi, na watawala wake wanao mwanga zaidi mioyoni mwao wa akili, ufahamu na uadilifu kuliko Pilato. Na mng'ao wa uadilifu wa serikali hii ni wa daraja ya juu kuliko wa serikali ya Kirumi. Basi, ni shukurani kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu kwamba Aliniweka katika kivuli cha himaya ya serikali hii ambayo mizani yake ya tahakiki ni nzito kuliko mizani yake ya shaka.

Ilmuradi, jina Masihi Mau'udi nililopangiwa huko mbinguni halimaanishi zaidi ya hii kwamba Mungu Mzima wa milele Amenifanya kuwa mfano wa Hadhrat Masihi[as] ili kwa amani na upole niwape watu uhai wa kiruhani. Sikulifasiri hivyo jina hili, yaani Masihi Mau'udi, leo tu, bali nilieleza maana hii hii miaka kumi na tisa kabla ya leo katika kitabu changu Baraahine Ahmadiyya.

Yawezekana baadhi ya watu wacheke juu ya maneno yangu haya au wanichukulie punguani na afkani, kwani mambo haya yanashinda ufahamu wa dunia, na dunia haiwezi kuyatambua, hususani Waislamu wa madhehebu ya zamani ambao wanazo kawaida za hatari kuhusiana na matabiri kama haya. Jambo hili linapaswa kukumbukwa kwamba madhehebu ya zamani ya Waislamu wanaomngojea Mahdi atakayetokana na kizazi cha Fatima[ra], mama yake Husain[ra]. Na vile vile wanamsubiri Masihi ambaye akiungana na Mahdi

atapigana na wapinzani wa Islam. Lakini nimesisitiza kwamba mawazo hayo yote ni upuuzi, batili na uongo, na wenye kuyaamini mawazo hayo wamekosea sana. Uwepo wa Mahdi wa namna hii wa kubunika umepenya mioyoni mwa Waislamu kwa ukosefu wa elimu na udanganyifu. Na ukweli ni huu kwamba Mahdi yeyote hatatokea katika Banii Fatima; hadithi zote kama hizo ni za kuzushwa, hazina msingi wowote, ni za kubuniwa zilizotungwa labda katika zama za utawala wa Waabasi. Na sahihi na ukweli ni huu tu kwamba ujio wa mtu mmoja kwa jina la Isa[as] umetajwa, ambaye hatapigana wala hatamwaga damu, na ataelekeza mioyo kwenye haki kwa unyenyekevu, umaskini, uvumilivu na kwa hoja zitoshelezazo. Hivyo, Mungu Amenipasha habari kwa kauli yake bayana na ishara zake wazi kwamba mtu yule ni wewe tu, na kwa kunisadikisha Ameshateremsha ishara za kimbingu na Amenidhihirishia siri za ghaibu na matukio yajayo, na Amenijaalia elimu za ndani ambazo dunia haizitambui. Na itikadi yangu hii kwamba Mahdi yeyote  mmwaga damu hatakuja duniani ni itikadi tofauti na Waislamu wote, nami nimeshasambaza itikadi hiyo katika Jumuiya yangu nzima na katika malaki ya watu, na ni kinyume cha matumaini ya Waislamu. Bila shaka itikadi zao zilikuwa za aina hii ambazo zilikuwa zinazalisha jazba za kinyama na kupeleka mbali na ustaarabu na ustahifu. Na mwenye kutafakari anaweza kuelewa kwamba mtu mwenye itikadi kama hizo ni mtu wa hatari. Basi, Mungu Aliye Rahimu na

Karimu, kwa njia ya kudhihiri kwangu Ameweka msingi wa kuleta suluhu, na kuoshelea mbali mioyo ya Jumuiya yangu na itikadi hizo za ovyo kama vile nguo inavyofuliwa kwa sabuni. Basi, hiyo ndiyo sababu kwamba watu hao wananichukia. Kama ambavyo sawa na matakwa ya Wayahudi, Hadhrat Masihi[as] hakuja akiwa mfalme, wala hakupigana na mataifa mengine, hatimaye Wayahudi walianza kumdhulumu, na wakasema huyu sio yule tuliyemsubiri, ndivyo ilivyozalika sababu hii hii hapa. Naam, kuna hitilafu zingine pia pamoja nayo. Watu hao wanayo itikadi hii pia kwamba sawa na uwezo wenu wachukieni watu wa mataifa mengine na kama nafasi ipatikane wahasirishwe pia. Lakini nasema kwamba mtu hawezi kamwe kuwa Mwislamu mpaka awahurumie wengine kama anavyojihurumia nafsi yake. Na nasaha yangu ni hii hii kwamba itakaseni mioyo na wahurumieni wanadamu wote na msimtakie ubaya yeyote, kwani ustaarabu mkubwa ndio huu tu. Ni masikitiko kwamba watu hao wanayo tamaa sana ya kulipiza kisasi kwa mataifa mengine. Lakini mimi nasema kwamba sameheni na acheni, na msiwe na kinyongo na tabia ya unafiki. Rehemuni ardhini ili mrehemiwe toka mbinguni. Na sikusema tu bali nimeonyesha kwa vitendo, nami sikupenda kamwe kunuia kumfanyia shari yule anayenuia kunifanyia shari. Kwa mfano, daktari Clark alinishtaki kwa jaribio la kumuua yeye, lakini shitaka hili halikuthibitika mahakamani, bali karina zilizalika

kinyume chake. Hapo Kapteni Douglas, Hakimu wa wilaya ya Gurdaspur, akaniuliza, 'Je, unataka kumshtaki Daktari Clark?' Nikasema kwa moyo mkunjufu, 'Hapana, bali mimi sikuwashtaki hata wale Wakristo pia waliothibitika kuwa wakosefu mahakamani. Kama kusamehe kusingekuwa imani yangu, basi baada ya kuudhika sana lazima ningeshtaki.' Kisha kupitia Anjuman Himayate Islam Lahore, Waislamu wa maeneo yale walitaka kumshtaki mwandishi wa kijitabu *Ummahatul Mu'miniin*, na kwa lengo hili wakampelekea kumbukumbu kadhaa Mhe. Luteni Gavana na wakaonyesha jazba sana, hata wakati huo pia nikapeleka kumbukumbu yangu kinyume chao. Nikaandika wazi wazi kwamba hatutaki kamwe kulipiza kisasi kwa mwandishi wa *Ummahatul Mu'miniin*; naam, faradhi yetu ni kuandika jibu lake la kimantiki. Hivyo, katika mambo hayo daima nimehitilafiana na watu hao na masheikh wao, jambo ambalo liliwahuzunisha sana; lakini sina uadui nao hata kidogo.[4] Na kwa vyovyote nawaona kuwa wenye kuhurumiwa. Na nani anaweza kuwa

---

[4] Tanbihi: Katika kesi ya Daktari Clark, Sheikh Muhammad Husain alipofika kama shahidi wa Daktari Clark, wakili wangu Sheikh Fadhl Din akaniomba ruhusa kumwuliza Muhammad Husain swali ambalo lingemfedhehesha sana Muhammad Husain mahakamani; nami nikamkataza na kumzuia kumwuliza swali kama hilo. Kama ningekuwa na uadui kwa yeyote duniani ningefanyaje hivi! Mwandisi.

mwenye kuhurumiwa zaidi kuliko anayeacha njia ya ukweli na usahihi. Kuna hitilafu moja kuhusu itikadi ya kifo cha Hadhrat Masihi[as], ambayo kwa sababu yake watu hao daima walikasirika. Nimeshathibitisha kwa utafiti mkubwa kwamba Hadhrat Masihi[as] ameshafariki. Nami nimeshapata ithibati madhubuti kwamba Mwenyezi Mungu Akimnusuru msalabani Alimtuma aende upande wa India kwa kuwaita Wayahudi waliokuwa wamesambaratika kwa kufukuzwa na Nebuchadnezzar, nao wakasakinia Faris, Tibeti na Kashmir. Basi, akikaa katika nchi hizo kwa muda fulani na kufikisha ujumbe wa Allah hatimaye akafariki Srinagar. Na kaburi lake tukufu lipo Srinagar katika mtaa wa Khanyar, linaloitwa kaburi la Nabii mwanamfalme Yus Asaf.[5] Jina la Yesu kama vile likawa Jesus, kwa kuchanganyikana na lugha tofauti likawa Yus Asaf.

Tawi la nne ni hili kwamba baada ya madai hayo, masheikh wa watu hao walinitendeaje? Maelezo yake ni

---

[5] Neno *jew* pamoja na majina ya baadhi ya makabila yenye heshimja ya Wakashmiri ni kumbukumbu ya kudumu inayothibitisha kuwa wao ni Wana wa Israeli, kwani maana ya *Jew* ni *Myahudi* tu. Na neno hili *Jew* limeundwa kwa maana hiyo katika Kiingereza pia. Zaidi ya ithibati hiyo madhubuti ya majina ya kaumu kufanana, Dakt. Bernier, mtalii maarufu Mfaransa, amethibitisha katika maelezo ya safari yake kwa hoja madhubuti na kwa ushahidi wa wahakiki wakubwa kwamba Wakashmiri kwa kweli ni wana wa Israeli. Mwandishi

haya kwamba baada ya kusikiliza dai langu la kuwa Masihi Mau'udi na kujua kwamba ninakanusha ujio wa yule Mahdi wao ambaye kumhusu yeye wameshatunga visa vingi vya kikatili na amekubaliwa kuwa mwenye kumwaga damu ovyo ardhini. Miongoni mwa masheikh hao, mtu mmoja Muhammad Husain aliye mhariri wa gazeti *Isha'atus Sunna*, mkazi wa Batala, wilaya ya Gurdaspur, aliandika fatwa kunikufurisha na alichukua saini za masheikh wengi juu yake. Akaniita kafiri na dajali, hata alitoa fatwa kwamba huyu anawajibika kuuawa; na kuteka mali zao ni halali, na kuchukua kwa nguuv wake zao na kuwaoa, mambo hayo yote ni sawa, bali yanasababisha kupata thawabu.[6] Basi fatwa hizo mbili zipo ndani ya tangazo la tarehe 29 Ramadhani 1308 Hijria lililochapwa katika Matbaa Hakkani, Ludhiana, na kwenye ukurasa wa nyuma ya kijitabu *Saife Masluul* kilichochapwa katika Matbaa Egerton, Rawalpindi, yaliyoandikwa kwa kuchochewa na Muhammad Husain. Lakini kwa hofu ya serikali ya

[6] Tanbihi: Muhammad Husain wa Batala, imani yake hasa ni hii hii kwamba Mahdi mwenye kupigana vita atakuja, lakini akiongopa anaiambia serikali hamwamini Mahdi wa aina hii ilihali mara kwa mara amedhihirisha kwamba anaamini. Kama serikali ikikusanya masheikh wengine iwaulize kwamba huyu mtu anawaelezea itikadi zake zipi juu ya Mahdi, basi itathibitika mara moja kwamba huyu mtu anasema nini mbele ya serikali na anawaambia nini ndugu zake, yaani masheikh wengine, juu ya Mahdi. Mwandishi

Kiingereza fatwa hizo zisipoweza kutekelezwa, ndipo Muhammad Husain alitumia hila nyingine kwamba mtu huyo asumbuliwe siku zote kwa matusi makali na kwa maneno ya kuudhi kama vile alivyodhihirisha mwenyewe katika sehemu kadhaa za gazeti lake *Isha'atus Sunna* la mwaka 1898.[7] Kwa kuendeleza shughuli hii ya kutukana na kutumia mdomo mchafu akaweka mtu mjanja anayeitwa Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli anayeishi Lahore. Na akiandika mwenyewe matangazo machafu ya aina aina, akayachapisha kwa jina la mtu huyo. Na kisiri Muhammad Husain mwenyewe alifanya kazi hii yote na aliendelea kuwaarifu watu juu ya kazi yake hii, na katika vitabu vyake pia aliendelea kunasibisha kwake kwa majisifu. Na matangazo hayo yote anayoendelea kutoa Muhammd Husain kwa ujanja na kwa lugha chafu tangu mwaka mmoja au zaidi kidogo, yanaandikwa kwa mtindo wa kihuni, kwa njia chafu sana mno. Na katika matangazo hayo hakuacha njia yoyote ya kunifedhehesha na kunidhalilisha. Ametaka kuharibu heshima yangu yote. Na matangazo hayo yanazo tuhuma chafu kiasi hiki kwamba siwezi kudhani kwamba mtu wa kaumu dhalili sana alimtendea mpinzani wake yeyote kwa ukali na kukosa haya. Kati ya matangazo hayo, tangazo moja ni la 12 Agosti 1898 ambalo lilichapwa katika matbaa ya

[7] Isha'atus Sunna, Na. 5, J. 18, uk. 146, 154, 155. Mwandishi

Fakhrud Din, Lahore, na vilevie tangazo la tatu, pamoja na nyongeza, la 11 Juni 1897, lililochapwa katika matbaa hiyo, naandika hapa madhumuni kiasi fulani, kwa mfano, ya hayo manne ili watawala wajue kwamba imenuiwa kiasi gani kunidhalilisha. Si mwezi mmoja wala miezi miwili, bali tangu mwaka mmoja anatoa matangazo machafu ambayo baada ya kujeruhiwa nayo mfululizo nililazimika kuandika tangazo tarehe 21 Novemba 1897[8] ambamo nimemwomba Mwenyezi Mungu Amdhalilishe mwongo. Na ndani ya matangazo hayo manne ya Muhammad Husain yaliyotolewa kwa jina la Ja'far Zatalli, kwa kunifedhehesha humo maneno makali sana na machafu na najisi yametumiwa. Yaani, imeandikwa kunihusu mimi, "Mke wa mtu huyu ana urafiki na baadhi ya wafuasi wake." Kisha kwa kimasihara akijiita mwenye kupokea ufunuo akaandika kuhusiana nami, kwamba amefunuliwa: "Mke wa mtu huyu ataolewa na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli." Na kisha kunihusu aliandika kidhihaka kwamba amefunuliwa kuwa: "Mkadiani akishikwa katika kesi ngumu atafungwa jela ya Kiingereza akitiwa pingu

[8] Sikuchapisha tangazo hilo la mubahala la 21 Novemba 1898 mpaka matangazo kadhaa kwa ombi la mubahala kutoka watu hao yakanifikia mfululizo. Zaidi ya matangazo hayo, barua moja ya Ja'far Zatalli ya tarehe 19 Novemba 1898 na matangazo matano mfululizo moja baada ya lingine, Muhammad Husain mwenyewe alisambaza juu ya ombi la mubahala.

miguuni, na atafukuzwa nchini. Na katika hali ya kufungwa atakuwa punguani na kurukwa na akili. Na litatokea banguzi sehemu ya chini ya mwili wake. Atakuwa mkoma, wadudu wengi watazalika mwilini mwake. Na sura yake itaborongeka kabisa. Na mke wake mpendwa atajenga urafiki na baadhi ya wafuasi wake, na kisha akiwa mzururaji atachukua talaka kwa Mkadiani. Na hatimaye ataolewa na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli, na Sheikh Abu Said Muhammad Husain atatangaza ndoa yake.[9] Na mwishowe Mkadiani akiwa kipofu, kiziwi na bubu na kwa kujiua ataingia jahanamu. Kisha Akaandika kidhihaka, "Funuo hizo zote zimeshatimia, ndoa peke yake imebaki." Kisha katika tangazo la tatu kimasihara akaandika kunihusu mimi, "Nimesikia kwamba mtu huyu ameshikwa na tauni na mbwa walikula nyama yake." Kisha katika toleo la Julai 1897 amechora picha yangu kama dubu.

Isitoshe, Muhammad Husain ameniita mara kwa mara mwovu, mhalifu wa serikali ya Kiingereza na muuaji katika *Isha'atus Suna* la mwaka 1898. Basi, dhuluma hii ya Muhammad Husain na kundi lake, yaani Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli na kadhalika ilipopita mipaka na nikadhalilishwa kiasi hiki kwamba hawakuacha neno lolote la dhila wasilolitumia kunihusu mimi, na kisha

[9] Sheikh Muhammad Husain ameandika kimasihara katika *Isha'atus Sunna* la mwaka 1898, "Nitatangaza ndoa ya mke wake kwa Muhammad Bakhsh."

walifululiza kuniletea ombi la mubahala. Hapo hatimaye nikatoa tangazo la 21 Novemba 1898 lililomaanisha hii tu kwamba kati ya makundi yetu mawili, Mwenyezi Mungu Alidhalilishe lile ambalo linaongopa. Kisha nikatoa maelezo bayana ya tangazo hili ndani ya tangazo la 30 Novemba 1898. Baada ya tangazo langu la 21 Novemba 1898 pia Muhammad Husain alitaka kuharibu jina langu na akatoa maana potofu ya tangazo langu la 21 Novemba 1898 kwamba humo nimemtisha kumuua ilihali katika tangazo hilo hilo nilieleza mara tatu kwamba 'tagazo hili ni kwa kudhalilika kwa mwongo tu, awe yeyote kati ya makundi yetu mawili. Kisha nikisikia kwamba Muhammad Husain anatoa maana isiyo sahihi ya tangazo la 21 Novemba 1898, nikatoa tangazo la 30 Novemba 1898 kwa lengo hili kwamba isije Muhammad Husain akawadanganya watu akitoa maana visivyo. Lakini nimesikia kwamba hata baada yake pia aliendelea kudanganya. Mtoto pia mwenye kipawa kidogo akiona matangazo yangu hayo mawili, ya 21 Novemba 1898 na ya 30 Novemba 1898, anaweza kuelewa vizuri kwamba katika matangazo hayo mawili hakuna utabiri wa kuuawa kwa yeyote, bali kuna dua na ufunuo tu kwa fedheha ya mwongo.[10] Na ndiyo sababu nilichapisha

[10] Ufunuo جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا ulioandikwa katika tangazo la 21 Novemba 98 unadhihirisha hii kwamba mwongo atadhalilika namna alivyomfedhehesha mtu wa kundi la pili. Basi, hapa namna dhila ndiyo mithili ya dhila iliyofanywa. Mwandishi

tangazo la Muhammad Husain lililotolewa kwa jina la Muhammad Bakhsh na Abul Hasan Mtibeti pamoja na tangazo langu la 21 Novemba 1898. Lengo langu lilikuwa ni hili tu kwamba ili ijulikane kuwa Muhammad Husain ametaka kunidhalilisha kwa kunitukana, nami nataka uamuzi huu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba aliye mwongo kati yetu adhalilike hivyo. Mwishoni mwa kijitabu hiki nimetoa tafsiri ya Kiingereza ya matangazo yangu mawili yaani la 21 Novemba 1998 na 30 Novemba 1898. Jambo hili kwamba kwa nini niliandika tangazo la 21 Novemba 1898 na kwa haja gani sahihi nilikuwa na haki ya kuliandika nimeshatoa jibu lake kwamba tangu zaidi ya mwaka mmoja nilipata kulengwa na matangazo machafu; yaani kutoka kwa Muhammad Husain na kundi lake matangazo ya matusi yaliendelea kutolewa mfululizo kunihusu mimi tangu mwaka mmoja. Na katika matangazo hayo nilitwezwa na kuondolewa heshima; na ilifanywa juhudi sana mno kwa kunidhalilisha kiasi hiki kwamba kina mama wa familia yangu walituhumiwa kwa uasherati na uzinzi, kwa shari ili kuleta ufisadi. Wakati wa mateso na dhila kiasi hiki inayoamsha ghera ya kibinadamu, ilikuwa ni haki yangu kwamba ningewashtaki mahakamani, lakini kulingana na njia yangu ya kidarweshi na subira sikushtaki. Na kwa mwaka mmoja takribani matangazo ya namna hii ambayo kila neno lake liliandikwa kwa kunifedhehesha, walinileteа Qadian Muhammad Husain na kundi lake

kupitia posta ilihali sikuwa mnunuaji wa magazeti na matangazo machafu kama hayo. Basi, nilipoudhiwa mara kwa mara kwa matusi na tuhuma za aina hii, hatimaye baada ya subira ya muda mrefu, kwa nia safi sana nilitoa tangazo la 21 Novemba 1898 lililokuwa na madhumuni hii tu kwamba Mungu Amfedheheshe mwongo jinsi alivyonidhalilisha.

Tawi la tano lifaalo kuelezwa ni hili kwamba kabla ya madai yangu, watu hao walikuwa na dhana gani juu yangu, na kwa nini baada ya madai wakwa na uadui kiasi hiki? Basi, hapa panatosha kuandika kiasi hiki kwamba Sheikh Muhammad Husain Batalawii, mhariri wa *Isha'atus Sunna*, aliye kiongozi wa wapinzani, alikuwa mwenye kunisifu sana mno kabla ya madai yangu hayo. Alikuwa akinifahamu kuwa mtu mwema, walii, fahari ya Waislamu na mwenye kuitakia heri sana serikali ya Kiingereza. Yeye aliandika juu yangu katika gazeti lake *Isha'atus Sunna* toleo la Juni, Julali na Agosit 1884, kwenye ukurasa wa 169 kwamba: "Mtu huyu amesimama imara kwa kuisaida Islam kwa mali, uhai, kalamu, ulimi na kwa hali na kauli kiasi hiki kwamba mfano wake umepatikana kwa nadra katika Waislamu wa hapo kabla." Kisha katika toleo hilo hilo kwenye ukurasa 176 ameandika: "Jinsi tunavyojua hali na fikira za mwandishi wa Baraahine Ahmadiyya (yaani mimi), watu wengine wa zama zetu watakuwa wachache sana. Bwana mwandishi ni ndugu wa kwetu bali mwenzi wetu shuleni pia katika ujana. Baba yake mheshimiwa Mirza Ghulam Murtadhaa

alithibitisha kwa vitendo katika uasi wa mwaka 1857 kuwa yu mwenye kuitakia heri serikali na kujitolea kwake na mtii wake, na akatoa farasi hamsini kuisaidia serikali." Kisha kwenye ukurasa 177 na 178 ameandika kwamba: "Bwana Mirza Ghulam Ahmad daima alijishughulisha kidarweshi kuitakia serikali ya Kiingereza heri, na mara kwa mara ameandika kwamba serikali hii ni kama baraka ya kimbingu kwa Waislamu. Na Mungu, Mwingi wa ukarimu, Ameituma serikali hii kama mvua wa rehema kwa Waislamu. Kupigana na serikali kama hii na kufanya jihadi dhidi yake ni haramu kabisa." Kadhalka Muhammad Husain alishuhudia waziwazi kunihusu mimi katika matoleo mengine kadhaa ya *Isha'atus Sunna* kwamba: "Mtu huyu ni mnyenyekevu, asiye na shari na ni mwenye kuitakia wema serikali ya Kiingereza." Naye alidumu miaka na miaka juu ya ushahidi huu mpaka wakati ambapo nilikanusha itikadi za watu hao zilizogandamana mioyoni mwao kwamba Mahdi atakuja duniani na atapigana na Wakristo, na kwa kumsaidia yeye Hadhrat Isa[as] atashuka kutoka mbinguni, na hatamwacha kafiri yeyote ardhini, na mali ya makafiri watapata masheikh na Waislamu wengine, na watapata mali kiasi hiki kwamba watashindwa kuitunza. Sikukubali visa hivyo vya upuuzi ambavyo havina msingi. Nikaandika mara kwa mara kwamba mawazo hayo hayathibitiki katika Hadithi wala Kurani, na ni upuuzi tu na batili kabisa. Si tu nilikataa, bali nilidhihirisha hii pia kwamba sawa na mpango wa Mwenyezi Mungu na kwa ufunuo

wake nimekuja kwa jina la Masihi Mau'udi. Nami nawadhihirishia watu kwamba itikadi hizi za Waislamu wa kawaida kwamba Mahdi atainuka kutoka kizazi cha Fatima[ra] na Masihi atakuja kutoka mbinguni kwa kumsaidia, kisha watapigana ardhini na makafiri na watapigana na Wakristo na kwa kuwazawadia masheikh na wenzao, mali nyingi itakusanywa, mawazo haya yote ni ya uongo na hayana msingi, bali mpiganaji yeyote vita za namna hii hatakuja. Ilikusudiwa kuwarekebisha walioghafilika kiroho tu, basi kwa urekebisho huo mimi nimekuja. Mawaidha yangu haya yaliwachukiza sana watu hao, kwani wamepata hasara ya mamilioni ya Rupia za kufikirika, nao wakakata kabisa tamaa ya kupata mali za mateka. Na badala ya Masihi Mau'udi na Mahdi, mtu mnyenyekevu amekuja anayekataza kupigana vita na anazuia njama chafu za uasi na anafundisha maisha ya umaskini. Basi mtu wa aina hii angewapendezaje! Wakawa hawana njia ila fatwa ziliandikwa kwa kumwua na kumsulubisha. Iliruhusiwa kidini kutwaa kwa nguvu wake zake na wanawake wa Jumuiya yake, na kuwaoa. Ilichukuliwa kuwa kitendo cha thawabu kutusi na kutuhumu, na kwa kumtaja mkewe kumtuhumu kwa tuhuma chafu. Kisha mara nyingine ghaidi na ghadhabu yao ilichemka ambapo Muhammad Husain alimsifu sana Sultani wa Rumi katika kijitabu chake, nami kinyume chake baada ya kuonana na Balozi wa Rumi nilitoa tangazo kwamba tunapaswa kuonyesha uaminifu na utii kwa serikali ya Kiingereza zaidi kuliko Sultani wa Rumi.

Serikai hii inazo haki zaidi juu yetu ambazo Sulatani hawezi kuwa nazo, kamwe hawezi. Kuhusu maandishi yangu haya masheikh walipiga makelele sana na kutusi vikali sana. Sir Seyid Ahmad Khan K.C.S.I. pekee akaafikiana nami kama vile nilivyoishaandika katika kijitabu hiki maneno yake aliyoyachapisha katika gazeti lake. Nasema kweli kabisa kwamba zaidi ya sababu hizo watu hao hawana sababu yoyote ya kuwa na uadui nami. Watawala waheshimiwa wa serikali ya Kiingereza wakisoma kwa makini matangazo ya watu hao wanaweza kutambua kwamba ukatili wa watu hao umefikia kiasi gani. Na mafunzo yangu ninayoifundisha Jumuiya yangu tangu miaka kumi na tisa hayawezi kufichika kwa serikali hii mhisani. Nimeishailazimisha Jumuiya yangu kwamba wasishindane na ubaya wa watu hao na waishi maisha kwa unyenyekevu. Nami nimejilazimisha pia kwamba ninyamaze juu ya tuhuma hizo chafu. Ndiyo sababu juu ya maneno yao ya kihuni ya watu hao mimi na Jumuiya yangu daima tulinyamaa. Mtu mwadilifu anaweza kuona kwamba njia hii ilikuwa kuudhi kiasi gani kwamba Sheikh Muhammad Husain kwa njia ya rafiki yake, Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli, alitoa tangazo dhidi yangu kwamba mke wa mtu huyu anao urafiki na watu wa Jumuiya yake, yaani ana uhusiano nao usio halali. Lakini nilinyamaza hata baada ya kusikia tuhuma hii. Kisha akaandika katika tangazo lingine kwamba nimesikia kwamba mtu huyu ameshakufa na mbwa wamekula nyama yake. Hata hivyo nikafanya subira. Kisha aliandika kunihusi mimi kwamba

tumefunuliwa kwamba mke wake akiwa mzururaji ataolewa na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli, na Muhammad Husain atatangaza nikaha yake. Hata hivyo nilifanya subira. Kisha katika tangazo lingine akiniita dubu, akachora picha ya dubu, akatia kamba shingoni mwake na akaandika matusi. Kisha katika tangazo lingine alidhihirisha ufunuo wake huu kwamba mtu huyu atafungwa jela na atapatwa na ukoma. Kisha huyu huyu Muhammad Husain aliandika katika sehemu fulani ya *Isha'atus Sunna* kwamba mtu huyu ni katili, mwovu na mwasi. Baada ya matangazo hayo yote watu hao waliomba kufanya mubahala mara kwa mara, na katika maombi hayo pia walitusi. Hatimaye kwa upole na ulainifu nilitoa tangazo la 21 Novemba 1898 lililokuwa na shabaha hii tu kwamba Mungu Amdhalilishe aliye mwongo kati yetu wawili. Lakini katika ufunuo sharti ya mithili imewekwa.

Ilmuradi, mpaka leo yaliyotokea baina yangu mimi na hao, hali yake ni hii tu niliyoeleza. Na matangazo yote machafu ya Muhammad Husain na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli ninayo ambayo madhumuni yake kwa muhtasari nimeshaandika katika kijitabu hiki. Na tarehe yao ya kuchapwa pamoja na jina la matbaa naandika hapa chini.

| **Tarehe ya Tangazo** | **Jina la Matbaa** | **Maelezo** |
|---|---|---|
| 11 Juni 1897 | Tajul Hind, Lahore, Takia Sadhwan | Kichwa cha maneno ya tangazo hili ni 'Nyongeza ya gazeti la Ja'far Zatalli.' Limeandikwa kwa kudokezwa na Sheikh Muhammad Husain Batalawii, Mhariri wa *Isha'atus Sunna* kama Sheikh mwenyewe alivyoishakubali katika gazeti lake *Isha'atus Sunna* na mbele ya mashahidi. Katika tangazo hili matabiri machafu sana yameandikwa. |
| 26 Juni 1897 | 〃 | Hili pia liliandikwa kutokana na kudokezwa na Sheikh Muha-mmad Husain. |
| 23 Juni 1897 | 〃 | Hili pia liliandikwa kwa dokezwa na Sheikh Muhammad Husain. |
| 26 Mai 1897 | 〃 | Katika tangazo hili tishio la uuaji pia limetolewa. |
| 20 Agosti 1898 | 〃 | Hili pia liliandikwa kwa kudokezwa na Muhammad Husain na limejaa matusi. |
| 7 Aprili 1897 | 〃 | Kwenye safu ya 3 ya ukurasa wa 4 imeandikwa kwamba Mirza ameshakufa na mwili wake umewekwa katika Jumba la makumbusho.[11] |

[11] Sio hii tu kwamba Muhammad Husain amekubali katika gazeti lake *Isha'atus Sunna* kwamba matusi hayo yote yametolewa kwa agizo lake na mafundisho yake, bali kuhusu jambo hili wapo watu wachache waheshimiwa mashahidi pia kwamba Muhammad

| | | |
|---|---|---|
| *Isha'atus Suna* la Muhammad Husain wa Batala, kuanzia mwaka 1891 hadi mwaka 1898 | | Katika majarida hayo yote kuanzia mwaka 1891 hadi 1898, Sheikh Muhammad Husain kwa namna zote alinituhumu na kutusi. Na alikiri hii pia kwamba matangazo yote machafu ya Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli yametolewa kwa dokezo la ishara yangu na kwa mafundisho yangu; na amemsifu sana Muhammad Bakhsh. |

Mwishoni jambo hili linapaswa kuzingatiwa na watawala kwamba mamia ya waheshimiwa na watu waungwana ni mashahidi juu ya maisha yangu safi, na pia Waheshimiwa viongozi wa Jumuiya yangu wanaoaminika sana na serikali. Kadhalika waheshimiwa machifu na wafanyabiashara wanaweza kutoa shuhuda juu ya mwenendo wangu mwema na mzuri. Na sitokani na ukoo uliotuhumiwa wakati wowote na serikali ya Kiingereza, wala yeyote hawezi kuthibitisha kwamba wakati wowote nilikutwa na hatia yoyote. Na katika Jumuiya yangu kuna viongozi wengi waheshimiwa, machifu, na wasomi waungwana ambao hawawezi kumfuata mtu mwovu yeyote. Na sina uadui binafsi na Muhammad Husain wala sina ushirika wowote naye wa mali; ni hitilafu ya itikadi za dini tu. Naam, kwa vile

---

Husain alikuwa akiwapa mswada wa matangazo hayo, ulioandikwa na mkono wake. Mwandishi.

watu hao wameshika tangu takriban mwaka mmoja mwenendo wao wa kutusi na kutoa matangazo machafu, kwa hiyo baada ya matangazo yao mengi yaliyoendelea kunifikia tangu takriban mwaka mmoja, na baada ya ombi lao la mara kwa mara la mubahala lililoombwa kwa kupitia matangazo, imeniongoza nia yangu nzuri, uchamungu na upole wangu kwamba badala ya matusi, nitake uamuzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya mubahala. Na njia hii ya mubahala sikuzusha mimi, bali hii inaendelea tangu zamani katika Islam kama suna. Hii ni njia ya Islam kwamba uamuzi usiowezekana wenyewe, Aachiwe Mwenyezi Mungu kwa njia ya mubahala. Lakini sikuandika kamwe tangazo hilo kwa ajili ya kifo cha mtu yeyote wala kwa msiba mwingine. Muhtasari wa tangazo ni huu tu kwamba kati ya watu wa pande mbili aliye dhalimu, Mwenyezi Mungu Amdhalilishe jinsi dhalimu alivyomdhalilisha mwenzake. Si kawaida yangu kamwe kwamba nitabiri mwenyewe kifo cha mtu yeyote. Watu wachache ambao kuhusiana nao utabiri ulitolewa hapo kabla, kama vile Deputy Atham na Pandit Lekhram, hao watu waling'ang'ania wenyewe na kwa kukazania sana walitoa maandishi yao yaliyoandikwa kwa mkono wao ambamo walisisitiza sana kwamba utabiri utolewe juu yao. Zaidi ya utabiri wangu, Lekhram alitoa utabiri dhidi yangu pia na alitoa tangazo kwamba mtu huyu atakufa hadi miaka mitatu kwa kipindupindu, na alisambaza utabiri wangu kwa ridhaa yake katika maelfu ya watu. Na kupitia

tangazo lake mwenyewe alidhihirisha kwamba utabiri huu umetolewa kwa ridhaa yangu. Na ni dhahiri kwamba mtu mpinzani kama Lekhram angewezaje kujizuia kunishtaki baada ya kusikiliza utabiri kama huo katika hali ya kukasirika. Mamia ya watu wanajua kwamba kwa kupata utabiri huo, yeye alikaa Qadian takriban miezi miwili. Kisha baada ya utabiri akaishi miaka mitano na hakupeleka shtaka popote kwamba utabiri huu umetolewa dhidi yangu pasipo ridhaa yangu. Hatimaye ndani ya muda wa utabiri, kwa ridhaa ya Mwenyezi Mungu, akaaga dunia. Hata wakati wa kufa pia hakuonyesha wasiwasi juu yangu, kwani alijua kwa moyo kwamba mimi si mwenye shari wala mwenye hila. Na yule anayesema kwa roho mtakatifu, je anafanana na yule mwovu anayetenda ubaya kwa udanganyifu wa kishetani na kufanya njama. Anayesema kwa matakwa ya Mungu, hawezi kuaibika mbele ya halaiki. Ni mahali pa shukurani maelfu kwamba tunaishi chini ya utawala wa serikali yenye huruma, uadilifu na busara. Kama hao masheikh wa kaumu yangu wanasaga meno juu yangu na wananidhania mwongo, mwenye vitendo viovu, basi naiweka serikali hii yenye hisani kuwa uamuzi baina yangu mimi na watu hao hivi kwamba nieleze habari yoyote ya ghaibu ya baadaye kwa kupata toka kwa Mungu, isiyohusika na wema au ubaya wa mtu wala isiwe na athari yoyote kwa mtu yeyote, na niiweke kuwa kigezo cha ukweli au uongo wangu, na nikiwa mwongo

nipewe adhabu ya kila aina; lakini ni nani kati yao aukubaliye uamuzi huu?

Ni masikitiko kwamba Muhammad Husain anatambua vizuri kwamba Lekhram alipata utabiri huo kwa kung'ang'ania sana na kwa lengo hili alikaa kwangu hapa Qadian kwa muda fulani. Na Deputy Abdullah Atham mwenyewe alijua kanuni za serikali. Basi ilikuwaje kwamba mtu aliyekuwa *Extra Assistant* aweze kunyamaza katika hali ya mimi mwenyewe kutoa utabiri. Na maandishi yake yaliyoandikwa na mkono wake nilitilisha pia ndani ya faili ya kesi ya Daktari Clark. Tena tangazo hilo la mubahala lililotolewa 21 Novemba 1898, ingawaje halihusiki na mtu yeyote bali limechapishwa kuhusu dhila ya mwongo tu. Nililichapisha asteaste na kwa tahadhari kiasi hiki kwamba nilizuia tangazo hilo kutoa mpaka yalinifikia mfululizo matangazo na barua kutoka kwa kundi la Muhammad Husain kwa kutaka kufanya mubahala. Matangazo hayo yote ya kutaka kufanya mubahala ninayo. Ilmuradi, hii ndiyo hali halisi niliyoeleza ya mambo yote yaliyotokea mpaka leo baina yangu mimi na kundi la Muhammad Husain.

Mwishoni mwa kijitabu hiki ninaweka matangazo yangu yote mawili, yaani tangazo la 21 Novemba 1898 na tangazo la 30 Novemba 1898, kwa kuzingatiwa na watawala.

Mwishowe naona lazima sana kuweka jambo hili mbele ya serikali yetu yenye hisani na yenye busara kwamba masheikh wa kaumu yangu wananichukia kwa sababu ninafundisha Jumuiya yangu kinyume cha matumaini na matarajio na matakwa yao. Aina ya Mahdi na Masihi waliomngojea, mimi napinga itikadi zile. Na Mwenyezi Mungu Amenidhihirishia kwamba mambo haya yote hayana asili na ni uongo kwamba Mahdi au Masihi atakuja duniani atakayemwaga damu kwa kueneza madhehebu na dini. Mungu hakutaka kamwe kueneza dini kwa njia hii. Kama katika zama za Mtume[saw] wetu vita vilipiganwa na wapinzani, vita hivyo havikuwa asilani kwa kueneza dini; vilikuwa kujitetea tu. Yaani, vilipiganwa kwa sababu wapinzani wa zama zile kwa chuki ya kijahili ya dini walitaka kuwatowesha Waislamu usoni mwa ardhi; waliendelea kuwaua na kuwaudhi sana na hawakuacha nafasi kwamba Islam itangazwe kwa uhuru. Basi baada ya matendo hayo ya uhalifu, watu hao wakauawa kwa kuadhibiwa – wale waliowaua Waislamu pasipo haki bila kosa lolote kwa chuki ya dini tu. Lakini sasa hakuna awauaye Waislamu kwa chuki na uadui wa kidini wala hakuna yeyote anayepigana nao kwa upanga kwa ajili ya dini. Naam, watu wa dunia wanapigana kwa mambo ya dunia wenyewe kwa wenyewe na waendelee, hatuhusikani nao. Basi, kwa kuwa hakuna yeyote anayeinua upanga kwa kuangamiza Islam, ni ujahili mkubwa na ni kinyume cha Kurani kuinua upanga kwa kisingizo cha kuisaidia dini. Kama mtu akija duniani

kwa jina la Mahdi na Masihi mmwagaji damu na awahamasishe watu kwamba piganeni na makafiri, basi yapasa mfahamu kwamba yu kadhabu na mwongo sana, na hatendi sawa na mafundisho ya Kurani bali anafuata njia iliyo kinyume chake. Nasema kweli kabisa kwamba wenye itikadi kama hizi hawafuati Kurani bali wanaiabudu sanamu ya mila ya kijahili na mazoea yao. Na huu ni ujahili wa mapadri pia na kosa kabisa kwamba bila haki wanapiga makelele siku zote kwamba katika Islam kusambaza dini kwa upanga ni amri ya Kurani. Na hivyo wanawaelekeza majahili wajinga kwenye mawazo ovyo na batili na kuwachochea. Watu hao hawana elimu ya Kurani wala hawafunuliwi na Mungu ili wapate elimu ya maana ya Neno la Mungu kutoka kwa Mungu, na hivyo wanaendelea kukumbusha bila haki jambo lisilo sawa. Mungu Amenijaalia elimu ya Kurani na Amenipa ufahamu wa kuelewa uteuzi wa maneno ya lugha ya Kiarabu hata kwamba nasema pasipo fahari kwamba katika nchi hii mtu mwingine yeyote hakupewa ufahamu kama huu. Nasema kwa nguvu kwamba katika Kurani hamna fundisho kama hili kwamba dini isaidiwe kwa upanga, au upanga uinuliwe dhidi ya wapinzani. Kurani inatufundisha mara kwa mara kwamba msubiri juu ya kuudhiwa na wapinzani. Basi inapaswa kuelewa kwa yakini kwamba Mahdi au Masihi wa aina hii hatakuja katika Islam atakayeinua upanga kwa ajili ya dini. Dini ya kweli inaingia mioyoni kwa hoja si kwa upanga; bali upanga unampa mpinzani

nafasi ya kupinga zaidi. Ni fadhili kubwa ya Mwenyezi Mungu kwamba kwa kufutilia mbali mawazo batili ya watu hao Amethibitisha ushukaji wa Masihi Mau'udi kutoka mbinguni kuwa kinyume cha ukweli, kwani kwa fadhili ya Mungu imehakikika hii kwa juhudi zangu. Na sasa watu wote watalazimika kuamini kwa sababu ya hoja madhubuti na matukio wazi wazi kwamba Hadhrat Masihi[as] hakwenda mbinguni kamwe na kiwiliwili chake. Bali sawa na ahadi ya Mwenyezi Mungu na kwa kukubaliwa maombi aliyoomba Hadhrat Masihi[as] usiku kucha kujiokoa uahi wake, akaokolewa msalabani na laana ya kufa msalabani. Akaja India, akajadiliana na watu wa dini ya Budha. Hatimaye akafariki katika Kashmir na lipo kaburi lake tukufu katika mtaa wa Khanyar, linalotambulika kwa jina la kaburi la Nabii mwanamfalme. Sasa asipoweza kuthibitika mwenye kuja kutoka mbinguni, bali ikathibitika kinyume chake, basi uwepo wa Mahdi pia umebatilika, anayetajwa kumwaga damu akiungana na Masihi[as]. Kwani sawa na kanuni ya utafiti na mantiki, kati ya vitu viwili vilivyolazimika kuwepo, kimojawapo killipobatilika basi na kitu cha pili pia kililazimika kubatilika. Kwa hiyo, imethibitika kwamba mawazo hayo yote ni batili, hayana msingi na ni upuuzi. Na kwa kuwa sawa na Torati, anayekufa msalabani anakuwa maluuni, na neno 'laana' lipo katika Kiebrania na Kiarabu ambalo maana yake ni hii kwamba maluuni aende mbali na Mungu na kumchukia Mungu, na Mungu naye Amchukie; na Mungu Awe adui

yake na yeye awe adui wa Mungu, hapo – Mungu Apishe mbali – hakuna mwenye kumheshimu kwa moyo atakayemtukana hivyo mpendwa wa Mungu kama huyo, mteule kama huyo, Nabii mtakatifu kama huyo aliye Masihi. Isitoshe, matukio yamethibitisha pia jambo hili kwamba Hadhrat Masihi[as] hakufa msalabani, bali akisalimika na mikono ya makafiri akaenda India kwa kujificha. Kwa hiyo, visa hivyo vyote vya hao masheikh wasiojua ni batili na matamanio hayo yote ya hatari ni upuuzi, na hakuna matokeo yake isipokuwa kwamba hayo ni mawazo ya kufitinisha. Kama itikadi za watu hao zikichunguzwa mahakamani kulinganisha na itikadi zangu, itajulikana kwamba watu hao wanazo itikadi za hatari namna gani, nao si tu mbali na ukweli, bali ni mbali na amani na njia ya usalama pia.

Na mwishowe nataka kumaliza kijitabu hiki kwa jambo hili kwamba ingawa sawa na itikadi za Kikristo ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Masihi hauhusikani na masilahi ya kisiasa, lakini jinsi masheikh wa Kiislamu wa siku hizi walivyoingiza katika itikadi zao kimakosa ushukaji wa Hadhrat Isa kutoka mbinguni na kupigana jihadi kwa kuungana na Mahdi, itikadi hii sio tu ya uongo, bali ni ya hatari pia. Na siku hizi uthibitisho niliopata wa ujio wa Masihi katika India na kufariki katika Kashmir unafutilia mbali mawazo ya hatari katika mioyo yenye busara. Na utafiti wangu huu sio wa muda mfupi wala si wa juu juu, bali umekamilika fika. Basi, chanzo cha utafiti huu ni marhamu ile inayoitwa marhamu ya Isa

nayo pia inaitwa *Marhamu Hawaariyyiin* –marhamu ya wanafunzi wa Yesu – na imetajwa katika vitabu zaidi ya elfu vya utabibu. Na matabibu Majusi, Wayahudi, Wakristo na Waislamu wameitaja katika vitabu vyao. Kwa vile sehemu kubwa ya umri wangu nimepitisha katika kusoma fani ya utabibu nami nimepata hazina kubwa ya vitabu pia, kwa hiyo nimepata dalili hii ya kuona kwa macho kwamba kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na kwa baraka ya maombi ya unyenyekevu, Hadhrat Isa[as] akisalimika msalabani na tena kwa sababu mbalimbali kwa kutumia *Marhamu Hawaariyyiin* akipona majeraha ya msalabani akaja upande wa India. Hakufa kamwe msalabani, alizimia tu na kwa mpango wa Mungu alikaa kaburini pia kwa siku tatu – katika kaburi lililokuwa kama chumba. Na kwa vile alikuwa mzima kama Yona, hatimaye akatoka humo.[12]

[12] Tanbihi: Jambo hili ni la yakini kwamba Hadhrat Isa[as] hakufia msalabani. Yeye mwenyewe akifananisha kisa chake cha kukaa kaburini kwa siku tatu na kisa cha nyangumi wa Nabii Yona, amemfahamisha kila mwenye busara kwamba aliingizwa kaburini akiwa hai kama Nabii Yona, na maadamu alibaki kaburini alikuwa hai, waila wafu wawezaje kushabihiana na wazima; na ni lazima mfano wa nabii usiwe upuuzi, usio na maana. Mahali pengine pia katika Injili jambo hili limeashiriwa ambapo pameandikwa kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu. Baadhi ya wanafunzi wa Yesu wanadhani kwamba Hadhrat Isa[as] alikufa msalabani, hii si sahihi kamwe. Kwani yeye kutoka kaburni, kuwaonyesha

Na asili ya pili ya utafiti huu ni vitabu vya kihistoria vya mataifa mbalimbali ambavyo kwavyo inathibitika kwamba lazima Hadhrat Isa[as] alikuja India, Tibeti na Kashmir. Na siku hizi mtalii mmoja Mrusi aliyethibitisha kuja kwa Hadhrat Isa[as] katika nchi hii, kwa kurejea vitabu vya dini ya Kibudha, nimekiona kile kitabu, nami ninacho hicho; kitabu hicho pia kinaunga mkono rai hii.

Na tena mwisho wa vyote, kaburi la nabii mwanamfalme lililopo katika Srinagar, mtaa wa

---

wanafunzi wake majeraha yake na kujifananisha na Nabii Yona, mambo hayo yote yanapinga dhana hiyo na ni kinyume chake.

Kisha wanafunzi wanahitilafiana pia kuhusu sehemu hii. Ndani ya Injili ya Barnaba niliyojionea mwenyewe kwa macho yangu, kimekanushwa kifo cha Hadhrat Isa[as] msalabani. Na ni dhahiri kutokana na Injili kwamba Barnaba pia alikuwa mwanafunzi mtawa. Na kwenda kwake mbinguni ni jambo la kiroho. Kinaenda mbinguni kile kinachokuja kutoka mbinguni; na aliye wa ardhi, anaenda ardhini. Torati na Kurani pia vimetoa ushahidi huu huu. Na kwa kuwa Wayahudi kwa sababu ya mpango wa kumtia msalabani, walikanusha kurufaika kiroho kwa Hadhrat Masihi[as], kwa hiyo walifahamishwa kwamba Hadhrat Masihi alikwenda mbinguni, yaani Mwenyezi Mungu Alimwokoa katika laana iliyokuwa tokeo la msalaba, akamwondolea lawama. Na ushahidi wa wanafunzi wachache unawezaje kukubalika ambao hawakubaki pale wakati wa tukio la msalaba, nao hawana ushahidi wa kuona kwa macho. Mwandishi.

Khanyar, ambalo watu wanaliita kaburi la mwanamfalme Nabii Yuz Asaf, na wengine kaburi la Nabii Isa Sahib, linaunga mkono maana hiyo. Na kaburi hilo lina dirisha moja pia ambalo mpaka sasa lipo kinyume cha makaburi yote ya dunia. Baadhi ya Wakashmir wanafikiri kwamba kuna hazina pia imezikwa pamoja na kaburi hilo, kwa hiyo kuna dirisha. Mimi nasema kwamba pengine kuna johari. Lakini ninavyofahamu, dirisha limewekwa kwa sababu kuna ubao adhimu wa maandishi ndani ya kaburi hilo. Jambo hili linaonekana kama ambavyo siku hizi katika wilaya ya Pirakoi iliyo kijiji kimoja katika wilaya ya mipaka ya Nepali ya nchi za Kaskazini Magharibi, sanduku zito limepatikana kutoka katika kilima fulani ambamo zilikuwemo johari, mapambo, mfupa na jivu; na kwenye sanduku iliandikwa kwamba haya ni mabaki ya mifupa iliyochomwa ya Gautam Buddha Shakyamuni. Na neno 'nabii' pia kuhusiana na mwenye kaburi linalotamkwa na maelfu ya Wakashmiri ni dalili moja ya madai yetu.[13] Kwani neno la nabii lipo katika lugha mbili za Kiebrania na Kiarabu; halipo katika lugha nyingine. Na ni itikadi ya Kiislamu kwamba baada ya Nabii wetu[saw]

---

[13] Kuna ushahidi mwingine juu ya madai yetu kwamba vitabu tulivyopata mpaka saa hii kuhusu historia na mafundisho ya Yuz Asaf ambaye kaburi lake lipo katika Srinagar, mafundisho yale yote yanafanana sana na mafundisho ya maadili ya Injili, bali baadhi ya mistari ni mistari ya Injili kabisa. Mwandishi

hatakuja nabii yeyote. Basi imethibitika kwamba huyo ni nabii miongoni mwa manabii wa Kiebrania. Na tena kwa kutafakari juu ya neno ‘mwanamfalme’ twaukaribia zaidi ukweli halisi. Kisha kwa kuona kuafikiana kwa wakazi wote wa Kashmir juu ya jambo hili kwamba huyo nabii ambaye kaburi lake lipo katika Kashmir alipita miaka mia sita kabla ya Nabii[saw] wetu, inaainisha wazi wazi kwamba huyo ni Hadhrat Isa[as], na inaamulika bayana kwamba huyo huyo ni Nabii Mtukufu na maasumu aliye mwanafalme wa kudumu kutoka arshi ya ujalali wa Mwenyezi Mungu ambaye Wayahudi wabovu wenye bahati mbaya walitaka kumwua msalabani.

Ilmuradi, huu ni uthibitisho ambao ikitazamwa hoja zake zote kwa pamoja, yanabatilika fika mawazo ya masheikh wabovu wa kaumu yetu, na jengo lenye baraka la amani na suluhu linaonyesha mng’ao wake – jambo ambalo natija yake ya lazima ndiyo kwamba hakuna yeyote aliyepaa mbinguni, wala hataleta makelele makubwa akiungana na Mahdi kwa kupigana vita, bali ameshalala kabisa mapajani mwa rehema ya Mungu wake katika Kashmir.

Wasomaji waheshimiwa, sasa nimeshadhihirisha misimamo yangu, miongozo na mafundisho mbele ya serikali yenye heshima. Muhtasari wa maagizo yangu ndio huu tu kwamba ishini kwa amani na upole, na serikali inayotutawala yaani serikali ya Uingereza muwe wenye kuitakia heri kikweli na kuitii, sio kwa unafiki na

kuipenda dunia. Hatimaye namaliza kwa kuomba dua kwamba Mwenyezi Mungu Amwongezee heshima siku hadi siku Malkia Mwadhamu Kaisari wa India, idumu heshima yake. Na Atujaalie tuwe watiifu wake kwa moyo wa kweli na tuwe wanadamu wenye kutaka amani. Amin

Mwandishi mnyenyekevu Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian

27 Desemba 1898

## Nyongeza ya Kitabu Hiki

## Kwa Kuzingatiwa na Serikali

Baada ya kuandika kitabu hiki nimepata kijarida kwa Kiingereza cha Muhammad Husain Batalawii wa *Isha'atus Sunna* ambacho akikichapisha katika matbaa ya Victoria Press, Lahore, alisambaza tarehe 14 Oktoba 1898. Nilihuzunika kwa kukisoma kijarida hicho, kwani amesema uongo wa kujiaibisha kuhusiana nami na kuhusu itikadi yake mwenyewe juu ya ujio wa Mahdi, na amejaribu kwa uzushi kabisa kwamba anidhihirishe kuwa mwasi machoni mwa serikali yenye heshima. Lakini sawa na methali hii sahihi na ya kweli kwamba 'Hakuna kitu chochote kilichofichika ambacho hatimaye kisidhihirike', nina yakini kwamba serikali yetu yenye akili na busara haraka itatambua hakika yenyewe ikoje.

Jambo la kwanza alilopeleka serikalini dhidi yangu kinyume cha ukweli katika kijarida chake ni hili kwamba anaiarifu serikali tukufu kuwa mtu huyu ni hatari kwa serikali tukufu, yaani moyoni anayo mawazo ya kuiasi. Lakini nasema kwa nguvu kwamba kama niko hivi basi napenda nife kuliko maisha ya utovu huu wa shukrani na uasi. Naielekeza serikali tukufu kwa adabu kufanya utafiti kamili iwezekanavyo kunihusu mimi na mafundisho yangu, na iwaulize kwa kiapo viongozi waheshimiwa maafisa wenyeji, machifu, waheshimiwa wengine na wasomi wa Jumuiya yangu ambao idadi yao inafikia mia kadhaa kwamba nimewapa maagizo gani

kuhusu serikali yenye hisani na nimewasihi kwa kuitii serikali hii kwa kusisitiza namna gani. Na vilevile serikali iangalie ushahidi wa sheikh huyu, yaani Muhammad Husain, alioandika kwa mkono wake katika gazeti lake, *Isha'atus Sunna,* uliotajwa katika kitabu hiki, kuhusu fikira zangu na fikira za baba yangu, Mirza Ghulam Murtadhaa, juu ya serikali ya Kiingereza wakati wa kutoa maoni juu ya kitabu changu, Barahiine Ahmadiyya. Na pia iangalie kwa makini maandiko yangu yanayoenezwa kwa kuisaidia serikali tukufu tangu miaka kumi na tisa mfululizo, na kunihusu mimi ifanye utafiti kwa kila jiha. Basi, kama hali zangu machoni mwa serikali zionekane za mashaka, basi nataka kwa moyo kwamba serikali initolee adhabu kali kabisa. Lakini kama Muhammad Husain huyo amefikisha taarifa hizo zote kinyume cha hali zangu za kweli, basi mimi nikiwa raia mtiifu, mwaminifu na mwenye kujitolea, naiomba serikali tukufu kwa adabu yote kwamba Muhammad Husain aulizwe kwamba kwa nini aliiarifu serikali kinyume cha ukweli mambo aliyoishakubali katika maoni yake juu ya Barahiine Ahmadiyya, hata kwamba kwa miaka kumi na miwili mfululizo hakudhihirisha rai yoyote tofauti na rai yake ya kwanza, na sasa ananiita mwasi katika siku za uadui, ilhali nimetumia kalamu yangu kuitakia heri serikali hii yenye hisani kwa miaka kumi na tisa na kufikisha upendo wa uadilifu wa serikali mpaka nchi za mbali kwa njia ambayo nasema kwa uthabiti kwamba mfano wa kazi hii hautapatikana

kamwe katika kazi za wengine. Sina maneno ya kueleza ombi langu la unyenyekevu mbele ya serikali kwamba mtu huyo ameniudhi kiasi gani kwa maneno yake yaliyo kinyume cha ukweli na jinsi nilivyopata majeraha ya kuumiza. Ni masikitiko kwamba mtu huyo amesema kwa kusudi uongo uliojaa dhuluma sana dhidi yangu mbele ya serikali na kutaka kuharibu huduma zangu zote. Ninazo sababu zilizo imara za madai haya na mashuhuda kamili na mashahidi. Natumai kwamba kwa sababu natokana na ukoo mwaminifu waliothibitisha utii wao kwa serikali kwa mali na uhai wao kwamba serikali hii yenye hisani itazingatia malalamiko yangu haya ya kuhuzunisha na kumkanya asemaye uongo.

Jambo la pili aliloandika Muhammad Husain katika kijarida hicho hicho ni hili kuwa kana kwamba nimetangaza ufunuo wa madhumuni hii ya kwamba utawala wa serikali tukufu utaangamia katika muda wa miaka minane. Niandike jibu lipi la tuhuma hii isipokuwa kwamba Mungu Amwangamize mwongo. Sikutangaza ufunuo kama huo. Vitabu vyangu vyote vipo mbele ya serikali. Naomba kwa adabu kwamba serikali imwamuru mtu huyu kusema kwamba katika kitabu au barua au tangazo gani nimechapisha ufunuo wa namna hii? Nami natumai kwamba serikali tukufu itatahadhari na hila yake, isije mtu huyo akapanga hila hii kwa kuthibitisha uongo wake huu kwa kuufikisha serikalini ushahidi wa uongo wa watu wa jumuiya yake na kundi lake wanaonichukia kwa sababu ya hitilafu ya

imani. Mtu huyu na wenzake hatutembeleani wala hatuonani ili niwaambie lolote kwa mdomo. Ninalotaka kusema nalichapisha katika vitabu na matangazo yangu. Na kwa kujua fikira zangu na funuo zangu, vitabu na matangazo yangu ndiyo ya kutegemewa, na wanajumuiya wangu waheshimiwa ni mashahidi. Ilmuradi, naomba kwa adabu kwamba serikali yetu tukufu imuulize huyu mtu juu ya taarifa yake ya uongo. Mheshimiwa Kapteni Douglas, Deputy Kamishna wa zamani wa wilaya ya Gurdspur, ameshaandika katika kesi ya Daktari Clark iliyosajiliwa dhidi yangu kwamba mtu huyo ananichukia, kwa hiyo haepukani hata kidogo na kusema uongo.

Jambo la tatu aliloandika Muhammad Husain katika kijarida hicho hicho ni kwamba mtu huyu anajidai kuwa Masihi Mau'udi. Kwa kujibu hili inatosha kuandika kwamba kama ulivyoendelea kuthibitika unabii wa Manabii[as], andivyo hivyo Alivyothibitisha Mungu wangu madai yangu haya, na ishara za kimbingu za Mwenyezi Mungu zimetoa ushahidi wangu. Sasa lililobaki ni kwamba kwa nini Muhammad Husain na masheikh wenzake wananiita mwongo na kwa sababu gani wananichukia kiasi hiki? Basi, nimeshaandika sasa hivi katika kitabu hiki kwamba chuki hiyo ni kwa sababu kwamba mafundisho yangu ni kinyume cha malengo na matakwa yao, yaani dhidi ya itikadi hii kwamba Masihi Mauudi atashuka kutoka mbinguni, akiungana na Mahdi

atapigana na Wakristo.[14] Na uwepo wa Mahdi ni muhimu katika itikadi yao kwa sababu Masihi Mau'udi hawezi kuwa Khalifa, kwani hayumo miongoni mwa Wakureishi, kama Muhammad Husain mwenyewe alivyodhihirisha jambo hili kuwa itikadi yake katika gazeti lake, J. 12, uk. 380, ndani ya hafla ya ukhalifa wa Sultani wa Rumi. Basi watu hao kwa hoja hiyo wakati wa ujio wa Masihi mara ya pili wameona haja ya Mahdi Mkureishi na kisha wametaja vita vingi pia. Na ninajua kwamba itikadi hizo ni za hatari sana, kwani mtu mwenye itikadi hiyo huwa na mipango moyoni mwake iliyo kinyume cha amani. Lakini mimi nazipinga itikadi hizo. Siamini Masihi wala Mahdi yeyote atakayepigana na makafiri na atawapa mali zao masheikh na kundi lao. Hivyo, machoni mwao, mimi ni mwongo kwani kwa

[14] Tanbihi: Kijarida alichochapisha siku hizi Sheikh Muhammad Husain, kwa lugha ya Kiingereza, mnamo Oktoba 1898, kwa kuionyesha serikali, ili serikali ya Kiingereza impatie sehemu ya ardhi, humo ameandika kinyume cha itikadi yake kwamba haamini ujio wa Mahdi Mau'udi ilhali kwa kukanusha kwangu imani hii hii ameniita mkana Mungu na dajali. Basi, amesema mbele ya serikali uongo huu wa kujiaibisha sana. Anawafundisha daima masheikh wenzake kwamba Mahdi Mau'udi atakuja na atapigana na Wakristo na Hadhrat Isa[as] atashuka kutoka mbinguni kwa kumsaidia; na mbele ya serikali anaeleza kinyume chake. Naomba kwa adabu kwamba serikali tukufu imfanye kutoa ushahidi wake mbele ya masheikh ili ukweli udhihirike anaoficha daima. Mwandishi

itikadi yangu matumaini yao yote yamevunjika. Nami nakubali kwamba mafundisho yangu haya yamehasirisha sana faida ya kufikirika. Lakini hili si kosa langu, bali ni kosa la matendo yao yasiyo sawa na kuelewa vibaya. Na kuandika kwa Muhammad Husain katika kijarida hiki kwamba haamini Mahdi yule ambaye masheikh wote wenzake wanamsubiri na kwa kumsaidia yeye, sawa na mawazo yao, Masihi atashuka kutoka mbinguni, hayo ni maandishi ya kiunafiki kabisa ambayo hayamo moyoni mwake. Na mamia ya masheikh wa Panjab na India wanaweza kutoa ushahidi kwamba anamwamini Mahdi mmwagaji damu, lakini kiunafiki anaeleza serikalini kinyume cha itikadi yake. Kama masheikh wenzake, kwa mfano Sheikh Ahmadullah wa Amritsar, Sheikh Rashid Ahmad wa Gangoha, Sheikh Abdul Jabbar wa Amritsar, Sheikh Muhammad Bashir wa Bhopal, Sheikh Abdul Haq wa Delhi, Sheikh Ibrahim Aarah, Sheikh Abdul Aziz wa Ludhiana na hususan Sheikh Nadhir Husain wa Delhi aliye mwalimu wa Muhammad Husain, waulizwe kwa kula kiapo kwamba mna itikadi gani juu ya Mahdi Mau'udi kwamba atakuja kwa kupigana vita au la, na vilevile je Muhammad Husain wa Batala, Mhariri wa *Isha'atus Sunna* ni miongoni mwenu na anafuata itikadi zenu au yeye hatokani nanyi, na je anapendekeza ukhalifa wa wakati huu nje ya Wakureishi, basi kwa mashuhuda haya hila zote hizi za unafiki za Muhammad Husain zitadhihirika mbele ya serikali kama ambavyo

kaburi lililopakwa rangi nyeupe na kupambwa vizuri linapofukuliwa mifupa na matumbo yanadhihirika.

Naihakikishia serikali yangu yenye busara na iliyotaalamika kwamba mtu huyu ana itikadi ile ile juu ya Mahdi ambayo wanayo marafiki wenzake, yaani masheikh wa Panjab na India. Serikali inaweza kuelewa kwamba inayumkinije kuwa Muhammad Husain akihitilafiana na masheikh wengine katika itikadi kubwa ya kiijma aweze kubaki kuwa rafiki na kiongozi wao. Na kuna dalili nyingine pia juu yake kwamba ameshaandika wazi wazi katika gazeti lake *Isha'atus Sunna*, J. 12, uk. 380, kwamba "Ukhalifa wa Wakureishi tu unakubaliwa; mtu wa kaumu nyingine hawezi kuwa Khalifa." Sasa inapaswa kufikiriwa kwamba huyu awezaje kuwa na maoni kwamba Hadhrat Masihi atakapokuja atakuwa mfalme, kwani yeye hayuko miongoni mwa Wakureish, bali yu miongoni mwa Waisraeli. Hivyo, katika hali hii vita vitapiganwaje bila uwepo wa Khalifa. Kwa hiyo, masheikh hao wote wamelazimika kukubali kwamba wakati wa ujio wa Masihi mara ya pili hakuna budi kuwepo Khalifa Mkureishi ambaye awe mfalme wa zama. Ndiyo sababu kwa kumkana Mahdi Mau'udi, itikadi zote za watu hao zinavurugika, na hata ujio wa Masihi kutoka mbinguni pia unakuwa upuuzi, kwani hakuna Khalifa wa kweli yeyote ardhini ambaye Hadhrat Masihi[as] akiungana naye apigane na makafiri. Kwa sababu hiyo, Muhammad Husain anaamini kwa moyo kwamba lazima wakati wa ujio wa Masihi, atakuja

Mahdi Mau'udi miongoni mwa Wakureishi atakayekuwa Khalifa wa zama, na Masihi Mau'udi, akiungana na wafanyao baiati ya Mahdi, atatoa huduma yake. Kwa hiyo, Hadithi اِمَامُكُمْ مِّنْكُمْ ya Sahihi Bukhari mbele ya watu hao kwa karina ya neno *Imamu* na karina ya neno *minkum* inaashiria kwenye Mahdi Mau'udi. Lakini, kwetu sisi hapa muradi wa Imamu ni Masihi ambaye anao Uimamu wa kiroho. Na rai yetu hii ni kinyume cha Muhammad Husain na masheikh wote wenzake wanaokaa katika Panjab na India, kwani neno Imamu lililomo katika Hadithi atakayetokana na Wakureishi na atapigana vita, na Masihi Mau'udi atakuwa mshauri wake, lakini Mahdi atakwua Khalifa wa zama. Ilmuradi, watu hao sawa na Hadithi اَلْاَئِمَّةُ مِنْ قُرَيْشٍ ambayo maana yake potofu imeshagandamana mioyoni mwao, wanayo itikadi hii tu kwamba hatimaye Ukhalifa utarudi katika Wakureishi na jina la Khalifa yule litakuwa Muhammad Mahdi atakayetokana na Banii Fatima na atamwaga damu nyingi kwa ajili ya dini.

Kama Muhammad Husain aulizwe hii tu kwamba sawa na itikadi yako wakati Masihi atakaposhuka kutoka mbinguni, hapo sawa na kauli yako Masihi hawezi kuwa Khalifa, kwani hatokani na Wakureishi, basi nani atakuwa Khalifa atakayepigana jihadi na makafiri? Na katika Hadithi ya Bukhari اِمَامُكُمْ مِّنْكُمْ Imamu ndiye nani, hapo watu hao hawatasema kamwe kwamba Imamu ndiye Masihi Mau'udi, bali watasema kwamba Imamu ni Mahdi, yaani yule atokanaye na Wakureishi. Basi, kwa

swali hili uhakika wote wa watu hao unafichuliwa. Inapaswa kutafakari kwamba katika hali ambapo Muhammad Husain hachukui Hadithi لَامَهْدِيَّ اِلَّا عِيْسٰى kuwa sahihi na anasema kuwa ndani ya Hadithi اِمَامُكُمْ مِّنْكُمْ ya Bukhari, Imamu siye Masihi Mau'udi, bali ni Khalifa atokanaye na Wakureishi, basi, je, maelezo hayo hayadhihirishi wazi wazi kwamba anamkubali Mahdi na anamsubiri? Katika hali hiyo mtu huyu anasema uongo wa kujiaibisha kiasi hiki kwamba anaielezea serikali ya Kiingereza itikadi tofauti na ile aliyo nayo mbele ya wenzake.

Kama watawala waheshimiwa wapange mazungumzo yangu na mtu huyu juu ya jambo hilo, na wakati wa mazungumzo masheikh wengine wenzake pia wasimamishwe hapo, mara moja itadhihirika kwamba mpaka sasa mtu huyu ameendelea kuidanganya serikali kinyume cha itikadi zake za moyoni mwake.

Ninayo maandishi yake ambayo kwa sababu yake wakati wa kuulizwa swali hilo atapata fedheha ile aliyoombewa mwongo kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika tangazo la 21 Novemba 1898.

Haifai kwa mtu yeyote kwamba aseme uongo kiasi hiki mbele ya serikali. Kama mtu huyu angekana ujio wa Khalifa Mkureishi anayeitwa Mahdi kwa maneno ya kawaida na angemwamini kama mimi kuwa Masihi yule ambaye hatapigana wala hatamwaga damu, basi

bila shaka yeye pia angeandikiwa fatwa ya kufuru kama mimi.

Naihakikishia serikali kwamba juu ya swala hili mtu huyu ana tofauti kubwa katika udhahiri na undani wake. Anawadhihirishia masheikh wenzake itikadi yake sawa na mawazo yao, na anapoandika kwa kuidhihirishia serikali hapo kwa kuifurahisha serikali anadhihirisha itikadi yake hii kwamba: "Siamini kwamba Mahdi yeyote atakuja na kupigana vita." Lakini, kama yeye hamwamini Mahdi, basi anaitwaje kuwa kiongozi na wakili wa masheikh wengine ambao wanamwamini Mahdi. Uamuzi wa kiadili wa mambo haya umo mkononi mwa serikali tukufu. Sawa na rai yangu, serikali itaweza kufikia uhakika wetu sisi wawili kwa urahisi kuhusiana na kesi hii kwa njia hii kwamba ichukue kauli yetu sisi wawili mbele yake na mbele ya masheikh wengine. Hapo mtu atakayekuwa na mwenendo wa kiunafiki, uhakika wake wote utadhihirika. Kwa hiyo, naomba kwa adabu kwamba jambo hili lazima liamuliwe. Aliposhikilia uongo huu dhahiri, basi yawezaje kutegemewa kwamba habari anazofikisha serikalini anasema kweli? Mwandihi.

**TAMATI**

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [15]

نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ [16]

Bishara yangu iliyomo ndani ya ufunuo wa 21 Novemba 1898, kuhusiana na mwongo, yaani ndani ya ufunuo ambao ibara yake ya Kiarabu ni جَزَاءُ سَیِّئَۃٍ بِمِثۡلِھَا

**IMESHATIMIA**

juu ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala.

**Naiomba serikali tukufu iangalie kwa makini tangazo hili.**

Maelezo ya kichwa hiki cha maneno ni haya kwamba sisi ni makundi mawili. Upande mmoja ni mimi na Jumuiya yangu na upande wa pili ni Sheikh Muhammad Husain na watu wa kundi lake yaani Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalii, Abul Hasan Tibeti na kadhalika … Muhammad Husain aliniita dajali, kadhabu, mkana Mungu na kafiri kwa sababu ya hitilafu ya kidini na akawashirikisha humo masheikh wote wa kundi lake. Na kwa sababu hii watu hao walikuwa wanatumia midomo michafu dhidi yangu na kunitukana vibaya. Hatimaye, baada ya kuudhika nilitoa tangazo la mubahala tarehe 21 Novemba 1898 ambalo ndani ya ibara yake ya ufunuo جَزَاءُ سَیِّئَۃٍ بِمِثۡلِھَا mlikuwa na utabiri

---

[15] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa na Ukarimu.

[16] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume.

kwamba kati ya makundi haya mawili, kundi linalodhulumu na kupita mipaka litafikiwa na dhila ya aina ile ile iliyofanywa kwa kundi lililodhulumiwa. Basi, leo bishara ile imetimia, kwani Sheikh Muhammad Husain Batalawii kwa maandishi yake alinidhalilisha hivi kwamba akiniita mpinzani wa itikadi ya kiijma ya Waislamu alinitangaza kuwa mkana Mungu, kafiri na dajali; na kwa maandishi ya namna hii akawachochea sana Waislamu dhidi yangu kwamba wasinitambue kuwa Mwislamu wala Ahli Suna, kwani itikadi zangu ni kinyume cha itikadi zao. Na sasa kwa kusoma kijarida cha mtu huyu cha 14 Oktoba 1898 alichochapisha Muhammad Husain katika Kiingereza kwa lengo la kuitumia kwa kupata sehemu ya ardhi kutoka serikali. Waislamu na masheikh wameshatambua kwamba mtu huyu mwenyewe ni mpinzani wa itikadi yao ya kiijima. Kwani katika kijarida hicho anakanusha kabisa ujio wa Mahdi Mau'udi anayengojewa na Waislamu wote ambaye sawa na mawazo yao atatokana na kizazi cha Hadhrat Fatima[ra] na atakuwa Khalifa wa Waislamu. Na vilevile atakuwa kiongozi wa dini yao na atapigana vita vya dini dhidi ya makundi mengine; na Hadhrat Isa[as] atashuka kutoka mbinguni kwa kumsaidia na kumwunga mkono, na wote wawili watakuwa na lengo moja tu, nalo ni hili kwamba wataeneza dini kwa kutumia upanga. Na sasa Sheikh Muhammad Husain ameshakanusha wazi wazi ujio wa Mahdi wa namna hii. Na kwa kukanusha huku sio tu amekanusha uwepo wa

Mahdi, bali amelazimika kumkanusha yule Masihi pia atakayeshuka kutoka mbinguni kwa kumsaidia Mahdi, na wote wawili wakiwa pamoja watapigana na wapinzani wa Islam. Na hii ndiyo itikadi ile ile ambayo kwa sababu yake Muhammad Husain aliniita dajali na mkana Mungu, na mpaka sasa alikuwa akiwadanganya Waislamu kwamba anaafikiana nao katika itikadi hiyo. Na sasa **pazia limeondolewa** kwamba kwa kweli anaafikiana na itikadi yangu yaani, anakanusha uwepo wa Mahdi na Masihi wa namna hiyo, kwa hiyo, amekuwa mkana Mungu na dajali machoni mwa Waislamu na masheikh wote. Basi leo bishara جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا imetimia kuhusiana naye, kwani hiyo ilimaanisha kwamba kundi dhalimu litapata adhabu sawa na ubaya ambao kwa kitendo lilifanya kwa kundi lililodhulumiwa.

Lililobaki ni kwamba ameniita mwasi wa serikali ya Kiingereza, basi kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu natarajia kwamba karibuni itaidhihirikia serikali kwamba kati yetu sisi wawili nani anafanya mambo ya uasi. Hivi karibuni kwa kumtaja Sultani wa Rumi akinishambulia ameandika makala ya hatari na uasi katika gazeti lake *Isha'atus Sunna,* Na. 3, J. 18 kwenye kurasa 98,99, na 100 ambayo muhtasari wake ni huu kwamba: "Yapasa kumtambua Sultani wa Rumi kuwa Khalifa wa kweli na kumkubali kama kiongozi wa dini. Na katika makala ile ameleta sababu moja hii kwa kuniita kafiri kwamba mimi simwamini Sultani wa Rumi kuwa Khalifa." Ingawa hii ni sahihi kwamba simwamini Sultani wa

Rumi kuwa Khalifa sawa na masharti ya Kiislamu, kwani yeye hatokani na Wakureishi, na makhalifa wa namna hii lazima wawe miongoni mwa Wakureishi. Lakini kauli yangu hii si kinyume cha mafundisho ya Kiislamu bali inaafikiana kabisa na Hadithi: اَلْاَئِمَّةُ مِنْ قُرَيْشٍ . Lakini ni masikitiko kwamba Muhammad Husain akitoa maneno ya kuasi ameachana na mafundisho ya Islam pia, ilhali hapo kabla mwenyewe pia alikuwa akisema kwamba Sultani sio Khalifa wa Waislamu wala sio kiongozi wetu wa dini. Na sasa kwa sababu ya uadui wangu, Sultani wa Rumi amekuwa Khalifa wake na kiongozi wa dini. Na katika mlipuko wa hamaki hakuijali hata serikali ya Kiingereza, na akadhihirisha yaliyofichika moyoni, na akamwita mwenye kuukana ukhalifa wa Sultani wa Rumi kuwa kafiri. Na alipata jazba hii yote kwa sababu niliusifu utawala wa Kiingereza na nilisema kwamba serikali hii sio tu inawahami Waislamu katika mambo ya dunia bali katika mambo ya dini yao pia. Sasa, kwa kueneza uasi anakanusha jambo hili kwamba Waingereza walituhami kidini kwa njia yoyote, na anasisitiza kwamba msaidizi wa dini ni Sultani wa Rumi pekee. Lakini huo ni uhaini kabisa. Kama serikali hii sio mlinzi wa dini yetu basi vipi tumesalimika na mashambulizi ya wakorofi. Je, jambo hili limefichika kwa yeyote kwamba wakati wa utawala wa Masingasinga hali ya mambo yetu ya dini ilikuwaje? Na namna gani damu ya Waislamu ilikuwa ikimwagwa kwa kusikiliza adhana tu ya sala. Sheikh yeyote

Mwislamu alikuwa hathubutu kumsilimisha Baniani yeyote. Sasa, Muhammad Husain atujibu wakati huo Sultani wa Rumi alikuwa wapi na alitusaidia nini wakati wa shida yetu ile? Basi, vipi amekuwa kiongozi wetu wa dini na Khalifa wa kweli wa Mungu? Hao walikuwa Waingereza tu waliotufanyia hisani kwamba mara baada ya kufika Panjab waliondolea mbali vizuizi hivyo vyote. Misikiti yetu ikajaa watu. Madrasa yetu yakafunguliwa na mawaidha yalianza kutolewa, na maelfu ya watu wa kaumu nyingine walisilimu. Hivyo, kama tuwe na itikadi hii, kama Muhammad Husain, kwamba tunawatii Waingereza kisiasa tu na kwa masilahi ya kidhahiri, yaani tunawatii kiunafiki, lakini mioyo yetu ipo pamoja na Sultani kwani yu Khalifa wa Islam na kiongozi wa dini, kwa kukanusha kuwa kwake khalifa na kwa kumwasi, mtu anakuwa kafiri, basi kwa itikadi hii bila shaka tutakuwa waasi tuliojificha wa serikali ya Kiingereza na waasi wa Mwenyezi Mungu. Ni ajabu, kwa nini serikali haifiki kwenye undani wa mambo haya, na kwa nini mnafiki kama huyo anaaminiwa anayeiambia serikali jambo fulani na anawaambia Waislamu jambo jingine. Naiomba serikali tukufu kwa adabu kwamba serikali tukufu ichunguze habari za mtu huyu kwamba namna gani anazifuata njia za unafiki. Na mawazo ya uasi aliyoshikwa nayo anayanasibisha kwangu.

Mwishowe, hakuna budi kuandika hii pia kwamba kiasi mtu huyu alichonitukana mimi na kumhamasisha

Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli kunitusi, na kunifedhehesha kwa uzushi wake wa aina aina, basi kilio changu ni mbele ya Mungu anayejua mawazo ya mioyo na ambaye mkononi mwake mna uadilifu wa kila mtu. Namwomba Mungu hii tu kwamba jinsi huyu mtu alivyonifedhehesha kunizushia uongo hata kwamba alieleza mambo kinyume cha ukweli mbele ya serikali tukufu kwa kunithibitisha kuwa mwasi, fedheha iyo hiyo impate yeye. Sikusudii kabisa kwamba apatwe na dhila tofauti pasipo dhila inayoafikiana na جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا[17]. Bali nikiwa katika hali ya kudhulumiwa nataka hii tu kwamba jinsi alivyonifedhehesha, ndivyo hivyo adhalilishwe ikiwa mimi niko mbali na tuhuma zile. Ingawa najua kwamba serikali hii ni stahimilivu na mara nyingi inasamehe; lakini kama mimi ni mwasi asemevyo Muhammad Husain, au jinsi nilivyogundua kwamba Muhammad Husain mwenyewe anayo mawazo ya uasi, hapo ni jukumu la serikali kwamba kwa kufanya uchunguzi kamili imwadhibu apasavyo atakayethibitika kuwa mwenye hatia kwa kweli ili usienee nchini uovu wa namna hii. Kwa kulinda amani, hii ndiyo njia rahisi sana kwamba masheikh maarufu wa Panjab na India waulizwe kwamba mtu huyu ambaye ni kiongozi na wakili wao anazo itikadi zipi? Na je itikadi anazowadhihirishia masheikh wa kundi lake ndizo zile zile anazoielezea serikali? Kwani ni lazima kwamba

[17] Sura Yunus 10:28

itikadi za masheikh ambao kiongozi na wakili wao ni huyu, pia ziwe zile zile ambazo ni za kiongozi.

Mwishoni, kuna jambo lingine la muhimu kwa kuzingatiwa na serikali kwamba Muhammad Husain amelichochea kundi lake dhidi yangu kwamba mtu huyu anapaswa kuuawa. Basi, kiongozi wa kaumu moja anapotoa fatwa[18] kunihusu mimi kupaswa kuuawa, hapo natarajia kwa uadilifu wa serikali tukufu kwamba jinsi anavyopaswa kutendewa kisheria, atendewe bila kuchelewa ili wafuasi wake kwa kupata 'thawabu' wasipange njama za kujaribu kuua. Basi.

Mwandishi mnyenyekevu Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian

27 Desemba 1898

***

---

[18] Tanbihi: Wakati wa kutoa fatwa hii ya kuua, Muhammad Husain amenituhumu akiongopa kwamba nimemdharau Hadhrat Isa[as], kwa hiyo napaswa kuuawa. Lakini huu ni uzushi mtupu wa Muhammad Husain. Katika hali nikiwa Masihi Mau'udi na ninashabihiana na Hadhrat Isa[as], kila mtu anaweza kuelewa kwamba, Mungu Apishe mbali, kama mimi ningemlaumu Hadhrat Isa[as], kwa nini ningesema ninashabihiana naye? Kwani, hivyo mimi mwenyewe nalazimika kuwa mbaya. Mwandishi